**ACT** yawasilisha barua kukutana marais, kusudio la kujitoa SUK
UKURASA 3

**POLISI** yamaliza Utata kuhusu kifo mwanafunzi
UKURASA 3



**KUELEKEA MIAKA 3** Rais Samia na msemo mcheza kwao hutunzwa
UKURASA 4




**SALAH AWEKA REKODI MPYA**
UKURASA 22


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumamosi Machi 16, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581617

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
Maoni@nipashe.co.tz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**WAZIRI APIGA 'STOP; UAGIZAJI NONDO NJE**
WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema Tanzania...

UKURASA WA 6

**SIMBA SC, YANGA JIPANGENI HAKUNA USHINDI 'MDOMONI'**
WAKATI Tanzania ikiwa imeweka rekodi ya kutoa timu...

UKURASA WA 9

**WALIA UTITIRI WA KAMPUNI BUBU ULINZI**
WAMILIKI wa kampuni binafsi za ulinzi wameomba...

**Mwalimu madrasa jela miaka 30 kwa kulawiti mwanafunzi**
UKURASA 3

# Mkanganyiko lishe waibua wataalamu

Wajifungia kutoa mwongozo kuokoa jamii....Endelea ukurasa wa 2



Prof Mohamed Janabi

## Kiingereza tatizo mtaala mpya elimu

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan, akiangalia zawadi ya picha ya viongozi wa nchi mbalimbali za Afrika, aliyokabidhiwa na Rais Yoweri Museveni wa Uganda baada ya mazungumzo yao, Ikulu ndogo Tunguu. Zanzibar juzi usiku. Viongozi hao, walizungumzia masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hususan umuhimu wa kuharakisha ukusanyaji maoni ya wananchi juu ya muundo na maeneo ya kuangaliwa katika Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la jumuiya hiyo, mchakato uliofanyika Burundi, Uganda na Kenya na kutekelezwa na timu ya wataalamu inayoundwa na wajumbe watatu kutoka kila nchi mwanachama. Kulia ni Rais William Ruto wa Kenya. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** YANGA YAWAPOTEZA MAMELODI CHAMAZI UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel John Nchimbi akizungumza na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. Viongozi hao, walizungumzia masuala mbalimbali yanayohusu uhusiano na urafiki wa kidugu kati ya chama hicho na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) na nchi hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkanganyiko lishe wawaibua wataalamu

**Na Romana Mallya**

MKANGANYIKO wa taarifa zinazotolewa na watu mbalimbali kuhusu lishe, umelishtua Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) na kuamua kuandaa mkakati utakaotoa mwongozo kwa Watanzania wale na kunywa nini kulingana na hali zao za afya.

Hatua hii inakuja baada ya hivi karibuni kuibuka baadhi ya madaktari, viongozi wa dini na wengine katika mitandao ya kijamii wanaojiita wataalam wa lishe, kila mmoja kutoa elimu yake kuhusu lishe, wengine wakikinzana kuhusu kitu ambacho mwananchi anatakiwa kukifuata.

Mmoja wa wataalamu ambao wamekuwa wakitoa ushauri mzuri kuhusu lishe bora na namna ya kubadili mtindo wa maisha kwa ajili ya afya bora ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi.

Mtaalamu huyo mbobezi, kutokana na ushauri huo, amekuwa gumzo katika jamii na amekuwa akiweka wazi kwamba hafanyi hivyo kwa kuchekesha au kufurahisha watu bali anasema ukweli mtupu.

Meneja wa TANCDA, Happy Nchimbi, alisema katika kusherehekea miaka 10 ya TANCDA mwaka huu, moja ya changamoto ni mkanganyiko wa taarifa za lishe zinazotolewa kwa wananchi.

"Jambo kubwa katika miaka 10 tunaloliona ni mkanganyiko hasa kwenye suala la lishe. Leo (jana) tumekutana na kukubaliana kwa pamoja tukae chini na tuangalie kitu gani tutoke nacho kama wadau na kumfikia mwananchi ili aishi salama na kutambua tunapoongelea lishe ni nini," alisema.

Alisema watakuwa na kikao ambacho kitaunda mkakati dhabiti wa kuhakikisha wanatoa elimu ya lishe iliyo sahihi na isiyo mchanganya mwananchi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu shirikisho hilo, Dk. Elisha Osati, alisema wamekutana kujadili mkakati wa namna ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza baada ya kuona madhara ni makubwa.

Alisema wamekutana zaidi ya vyama 20 vinavyojihusisha na magonjwa hayo kwa kuwa sasa wanaona kuna ongezeko kubwa la matatizo hayo.

"Tumeona mgogoro wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuhusu malipo au gharama za huduma na unagundua magonjwa mengi ni haya yasiyoambukiza. Hata kwenye familia gharama zinakuja kubwa.

"Tunatengeneza mkakati wa pamoja ili tuweze kutoka nao ili kufikia wafanya maamuzi. Jambo moja ambalo tunaona limeleta mkanganyiko hivi karibuni ni suala la lishe kwa kuwa, mambo mengi yanatokana na lishe.

"Kwa bahati mbaya wazungumzaji wamekuwa wengi kidogo kwenye suala la lishe huyu anakwambia ule huyu anakwambia usile, hili ni jambo moja kubwa tunalojadili leo (jana)," alisema.

Dk. Osati alisema lengo la majadiliano hayo ni kuwa na mkakati wa pamoja namna ya kuwaambia watanzania kama wataalam, mtu ale namna gani kulingana na hali ya ugonjwa, kazi na uzito alionao.

Mtaalam huyo alisema wameona namna ya ulaji wa chakula na unywaji ndiyo inayoleta matatizo hayo makubwa ya magonjwa yasiyoambukiza.

Alikumbusha kuwa suala la magonjwa yasiyoambukiza huchangiwa na mambo mengi yakiwamo chakula, unywaji na mtindo wa maisha.

Dk. Osati alisema kwa sasa wameanza kutengeneza mkakati wa ndani na baadaye watashirikisha wadau wengine ikiwamo serikali na kabla ya mwaka huu kuisha wawe wamefanya kikao cha pamoja cha kuwa na ujumbe wa pamoja kuhusu masuala ya lishe.

Dk. Waziri Ndonde, ambaye ni Mtaalam wa Afya na Mazoezi kutoka TANCDA, alisema shirikisho hilo lilianza mwaka 2014 na mwaka huu linatimiza miaka 10.

Shirikisho hilo, alisema linajivunia namna lilivyowaweka pamoja wataalam, watoa huduma za afya pamoja na wagonjwa husika kufikia ajenda ya magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema vyama vya magonjwa yasiyoambukiza vimesaidia Wizara ya Afya katika ufanyaji kazi. Awali, hakukuwa na Idara ya Magonjwa Yasiyoambukiza lakini 2019 iliundwa rasmi na kuzinduliwa na Waziri Mkuu.

# NIDA yaongeza kasi utoaji vitambulisho

**Na Agnes Gerald, NIDA**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imepongezwa kwa juhudi kubwa inayofanya ya kuchapisha vitambulisho vingi vya taifa na kuvisambaza kwa wananchi na hivyo kumaliza kero sugu ya upatikanaji wake kwa wananchi.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, wakati kamati ilipofanya ziara katika Kituo Kikuu cha Kuchakata na Kutunza Taarifa za Watu cha kukagua mradi wa vitambulisho NIDA jana.

"Kamati tumefurahishwa sana na jitihada za Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti na watumishi wote wa NIDA katika kuhakikisha mnafikisha malengo ya kuzalisha Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi waliokuwa wamesalia zaidi ya milioni kumi. Hakika mmefanya kazi nzuri na mnastahili pongezi za dhati," alisema Kawawa ambye pia ni Mbunge wa Namtumbo.

Alisema tatizo la kutopatikana kwa vitambulisho ilikuwa kilio cha wananchi kila kona lakini sasa wamevizalisha vingi na kuvipeleka kwa wananchi katika mitaa, vijiji na vitongoji vyao.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, katika taarifa yake kuhusu utekelezaji wa mradi wa vitambulisho hivyo iliyowasilishwa kwa niaba yake na Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Mhandisi Ismail Rumatila, alisema hadi mwezi Februari, mwaka huu, mamlaka imechapisha vitambulisho 20,548,067 na 19,743,367 kati ya hivyo vimesambazwa.

Alisema kasi ya uzalishaji na usambazaji imeongezeka kutokana na serikali kutoa fedha za ununuzi wa kadighafi 13,514,251 ambazo zinatumika kuvizalisha vya watu wote waliokwishasajiliwa na kupata Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN).

Ameishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa NIDA zilizowezesha kununuliwa kwa kadighafi hizo na hivyo kuchapisha vitambulisho kwa wingi na kuvisambaza kwa wananchi.

Kuhusu kuboresha na kuongeza njia za uhakiki na utambuzi, Sagini alisema NIDA inaandaa mkakati kwa kuongeza uhakiki wa kutumia alama ya mboni za macho na sura ili kuwezesha utambuzi na uhakiki kwa watu wasiokuwa na alama za vidole.

# Kiingereza tatizo ufundishaji mitaala mipya

Na **Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET) imesema moja ya matatizo waliyobaini katika kufundisha kupitia mitaala mipya ni wanafunzi kushindwa kujifunza lugha ya Kiingereza kutokana na kutawaliwa na lugha mama.

Katika mtaala mpya wa elimu ulioanza kutumika kuanzia Januari, mwaka huu, wanafunzi wanafundishwa Kiingereza kuanzia darasa la kwanza.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dk. Aneth Komba, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akijibu maswali na kutoa maelezo kwa Kamati Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ilipotembelea taasisi hiyo.

Alitoa kauli hiyo baada ya wabunge kuhoji kuhusu changamoto zilizojitokeza kwenye kuanza kutumia mtaala huo unaofundisha masomo kwa Kiingereza kuanzia darasa la kwanza na kutaka pia utafiti zaidi ufanyike.

Dk. Komba alisema wanafunzi wanashindwa kujifunza Kiingereza kwa wepesi kutokana na kuzoea ya asili au lugha mama, hivyo TET imelitafutia ufumbuzi kwa kutumia ujuzi kutoka nchini Uingereza kwa kupokea wataalamu.

"Majaribio yataanzia katika shule chache ambazo zimeainishwa zikiwamo za Morogoro. Wanafunzi wataanza kufundishwa wakiwa na miaka mitano" alisema.

Dk. Komba alisema wabobezi hao watatoka Taasisi ya Jolly Foundation ya Uingereza na programu itakayotumika inaitwa 'Jolly Phonics' na kwamba wataanza kwa majaribio na baada ya mafanikio yake itaendelea nchi nzima katika maeneo yenye ugumu huo.

"Wataalamu hao wataleta ujuzi na njia bora ya kufundisha watoto kusoma na kuandika Kiingeraza" alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuanzia sasa TET itaanza kuandaa vitabu vyote vya mtaalam mpya kielektroniki na wanafunzi watasoma kwenye kompyuta, vishkwambi na simu janja.

"Kwa kushirikiana na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), TET inakamilisha maandalizi ya 'TET Education Platform' ambayo itaandaa vitabu vyote kidijitali na mwanafunzi atasoma na kujibu maswali kielektroniki," alisema.

Pia alisema kutakuwa na kitu kama kitufe (buzz) ambacho kama anasoma na kujibu maswali kitakuwa kinatoa sauti iwapo amepata jibu au amekosea.

Kuhusu wanafunzi wenye mahitaji maalumu kama kusikia na kuona, alisema kuna 'app' au moduli itakawawezesha kufikia na kutumia vitabu vya kielektroniki.

Aidha, alisema taasisi yake inawasiliana na kampuni za simu ili kuondoa gharama na kwamba, wanafunzi watasoma vitabu hivyo bila kuwa na bando wala kulipia gharama za vifurushi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, alisisitiza TET kufanya utafiti na kuibua zaidi changamoto za kufundisha mitaala mpya ili zipate ufumbuzi.

# Polisi yamaliza utata wa kifo cha mwanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HATIMAYE Jeshi la Polisi, limejitokeza hadharani kumaliza utata kuhusu madai ya kutaka kupotezwa kwa haki za mwanafunzi wa darasa la kwanza wa Shule ya Msingi Mrupanga iliyoko Uru, wilaya ya Moshi, Janathan Makanyaga (6), anayedaiwa kufariki dunia baada ya kucharazwa bakora na mwalimu wake.

Uchunguzi wa jeshi hilo, umebaini kuwa baada ya mwanafunzi huyo kuadhibiwa, alipelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) Februari 28, mwaka huu, bila kutolewa taarifa polisi.

Baada ya kufikishwa hospitalini hapo, inaelezwa Jonathan alifariki dunia Machi 11, mwaka huu wakati akipatiwa matibabu.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP) Simon Maigwa, alisema tayari jeshi hilo linawashikilia walimu watano tarajali, waliokuwa katika mafunzo ya vitendo kwa ajili ya mahojiano.

"Tunawashikilia baada ya kuripotiwa na bibi wa mwanafunzi aitwaye Janathan Stephan Makanyaga (6), mwanafunzi wa darasa la kwanza wa Shule ya Msingi Mrupanga, kuhusika na kifo cha mwanafunzi huyo.

"Inadaiwa mwanafunzi huyo, aliadhibiwa na walimu hao kwa fimbo Februari 28, 2024 kisha kupelekwa Hospitali ya Rufani ya KCMC bila kutoa taarifa Polisi, na alifariki dunia 11/3/2024 akiwa anapatiwa matibabu hospitalini hapo. Jeshi la Polisi lilipokea taarifa za kufariki kwa mwanafunzi huyo tarehe 11/3/2024 na kuanza uchunguzi mara moja ikiwa ni pamoja na kukamatwa kwa walimu hao," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa, mwili wa Jonathan umefanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya maziko.

Alisema uchunguzi kuhusina na tuhuma hizo umekamilika na shauri hilo limepelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), kwa ajili ya kulitolea uamuzi. Inaelezwa kwamba chanzo cha kuadhibiwa mwanafunzi huyo ni kuchelewa kuwahi kushika namba.

Baadhi ya vyanzo vya taarifa vinaeleza kuwa mwanafunzi huyo alipoingia darasani alianza kutokwa damu puani na mdomoni.

Katika tukio lingine, Polisi inamshikilia mtuhumiwa mmoja (jina limehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi) na wengine wanaendelea kutafutwa kwa tuhuma za mauaji ya Hussein Mrutu (19), mkazi wa Mtaa wa Sadini, Kata ya Makuyuni, Moshi.

Kamanda Maigwa alisema mauaji hayo yalitokea Machi Mosi, mwaka huu, na kwamba siku ya tukuio, inadaiwa kulitokea ugomvi kati ya Mrutu na watuhumiwa hao wakiwa wanakunywa pombe katika baa ndogo ya Museveni na kusababisha mauaji hayo.

# ACT yawasilisha barua kukutana na marais kusudio la kujitoa SUK

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Uongozi ya Taifa ya Chama cha ACT Wazalendo imesema imewasilisha barua ya maombi ya kukutana na marais Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuhusu kusudio la kujitoa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar.

Chama hicho kimetishia kujindoa kupitia azimio la Halmashauri Kuu kwa kile kilichosema endapo mambo matatu waliyokubaliana kati ya Rais Mwinyi na marehemu Maalim Seif Sharif Hamad hayatofanyiwa kazi kwa muda uliobakia.

Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho Zanzibar, Ismail Jussa Ladhu, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya chama hicho, Vuga mjini Zanzibar.

Jussa alitaja mambo hayo kuwa ni kuundwa Tume Huru ya Kimahakama ya Uchunguzi kuhusu uvunjwaji wa haki za binaadamu, matukio yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ili watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria.

Jambo la pili, alisema ni mfumo wote wa uchaguzi ukijumuisha na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) na sekretarieti yake ya sheria ya uchaguzi na sheria zingine zinazosimamia vyombo vinavyohusika na uchaguzi kufanyiwa marekebisho ili kuwa na uchaguzi huru, haki na amani.

"Jambo la tatu ni kuanzishwe tume ya kudumu ya maridhiano na umoja wa kitaifa itakayosimamia kazi ya kujenga, kuendeleza na kuimarisha maridhiano na umoja wa kitaifa kutoka ngazi ya taifa hadi ngazi ya chini waliopo wananchi," alisema.

Jussa alisema chama hicho kinataka utekelezaji wa vitendo kuhusu makubaliano hayo kwa mustakabili wa nchi na wananchi wa Zanzibar katika kulipeleka mbele taifa la Zanzibar.

"ACT wazalendo imetoa muda wa kutosha kwa Rais wa Zanzibar kuhusu kutekeleza makubaliano hayo, lakini mpaka sasa hakuna nia njema ya utekelezaji wa mambo hayo ambayo ndio yalifanya ACT kukubali kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema.

Alisema licha ya chama kukumbusha mara kadhaa suala hilo, lakini mpaka sasa Chama cha Mapinduzi Zanzibar kinaonesha hakina nia njema ya utekelezaji wa makubaliano.

Jussa alisema Maalim Seif alipowasilisha hoja hizo kwa Rais Mwinyi aliyakubali lakini badala ya kuyaweka masharti ya kutekelezwa kabla ya kujiunga na serikali, watayatekeleza kwa kushirikiana pamoja wakiwa wote ACT Wazalendo na CCM wakiwa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. "Mbali na mambo hayo kutofanyiwa kazi, kudhihirisha kuwa hakuna nia njema kumekuwa kukifanyika vitendo vinavyokwenda kinyume na dhamira ya kujenga maridhiano na umoja wa kitaifa kwa mifano kadhaa ambayo tunayo,"alisema Jussa.

Alitaja baadhi ya mifano ambayo aliita ni kinyume cha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni pamoja na uteuzi wa madiwani nchi nzima ambapo hakuna hata diwani aliyetoka ACT Wazalendo.

Pia alisema uchaguzi ndogo katika majimbo ya Pandani, Konde, Kinuni, Amani, na Mtambwe yalihusisha matukio yale yale kama ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 yakiwamo matukio ya kuteka wanachama na mawakala wa ACT Wazalendo.

Kadhalika alisema kuteuliwa Thabit Idarous Faina, kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi, ambaye wanadai ni kinara mkuu aliyehusuka kuuchafua uchaguzi wa mwaka 2020.

"Wananchi wanatakiwa kujua kuwa mambo yote ACT Wazalendo inayodai na makubalino yaliyofikiwa kati ya Rais Mwinyi na Maalim Seif hakuna hata moja linalohusu maslahi ya chama, bali yameangalia zaidi maslahi ya wananchi za Zanzibar kwa ujumla," alisema.

Jussa alisema katika kujikwamua hapo walipofika ni lazima mambo hayo matatu yatekelezwe kikamilifu na kuwapo kwa ratiba ya utekelezaji wake na kukamilika ndani ya miezi sita ijayo.

Aidha, Jussa alisema utekelezaji na baadhi ya hatua uanze mara moja ili kujenga imani na nia thabiti na malengo ya dhati ya makubaliano hayo. "Iwapo hakutokuwa na muafaka kuhusu makubaliano hayo chama hakitosita mara moja kuchukua hatua ya kujiondoa katika serikali," alisema.



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo Dorothy Semu akisalimiana na Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Abdulrahman Kinana, baada ya kikao cha viongozi wa Kituo Cha Demokrasia Tanzania, jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Zanzibar, Ismail Jussa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwalimu madrasa jela miaka 30 kwa kumlawiti mwanafunzi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela, aliyekuwa mwalimu wa madrasa katika Msikiti wa Ushirika wilayani hapa, Abdala Selemani (37), baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mwanafunzi wake wa kiume mwenye umri wa miaka 12.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Nasra Mwashee ambaye alisema mahakama imeridhika bila kuacha shaka na ushahidi uliotolewa kuhusu kitendo hicho ambacho ni kinyume cha kifungu cha sheria namba 154(1) (a) cha Kanuni za Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alisema adhabu hiyo itakuwa fundisho kwake na watu wengine wenye tabia ya kufanya vitendo hivyo vya kikatili kwa watoto kwenye jamii na kuongeza kuwa ukatili kwa watoto hasa ubakaji na ulawiti, vimekuwa vikitokea mara kwa mara kwenye wilaya ya Nzega na adhabu hizo zitakuwa ni fundisho kwa wengine.

Awali, Wakili wa Jamhuri, Jenipha Mandago, aliiambia mahakama hiyo kwamba Selemani alitenda kosa hilo Oktoba 15, 2023 majira ya saa 10:00 jioni baada ya kuwekewa mtego kwa kuwa alikuwa akiwalawiti watoto mara kwa mara ambao alikuwa akiwafundisha elimu ya dini katika msikiti huo.

Alisema tukio la kumlawiti mtoto huyo wa miaka 12 mwanafunzi (jina na shule vinahifadhiwa) alilifanya eneo la chooni na kumsababishia mtoto huyo maumivu makali mwilini.

Mandago alidai kwamba kutokana na kosa alilolitenda, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye nia na tabia kama hizo kwenye jamii, ambao wanawatendea vitendo vya kikatili watoto.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, mahakama hiyo ilitoa nafasi ya utetezi kwa Selemani iwapo itamtia hatiani na kuomba apunguziwe adhabu kwa kuwa ana familia ya watoto wanne na mke ambao wanamtegemea.

Hata hivyo, mahakama haikuridhika na utetezi huo, hivyo kumhukumu kwenda jela akatumikie kifungo cha miaka 30.

# Samia na msemo mcheza kwao hutunzwa

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

**HAWAKUKOSEA**

WAHENGA waliosema mcheza kwao hutunzwa, hawakukosea. Hii ni baada ya wananchi wa Kijiji cha Kizimkazi anakotoka Rais Samia Suluhu Hassan, kusema Kizimkazi ya sasa ni tofauti na ile ya kabla miaka mitatu ya uongozi wake.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi hao wanasema Kizimkazi ya miaka mitatu iliyopita haikuwa kama ilivyo sasa katika nyanja za uchumi na maendeleo, afya na elimu.

Zakia Ali, mkazi wa kijiji hicho, anasema katika sekta ya afya ujenzi mkubwa wa hospitali unaendelea na kumalizika kwake kutawafanya wananchi kuondokana na tatizo la kufuata huduma masafa marefu.

"Licha ya kujengwa hospitali kubwa ambayo bado ujenzi wake haujakamilika, tumeboreshewa kituo cha afya na huduma za awali zinapatikana. Tuna imani kwamba kabla Rais Samia hajamaliza awamu yake ya kwanza, ujenzi wa hospitali kubwa ya kisasa utakuwa umekamilika," anasema.

Hata hivyo, anasema kuna baadhi ya huduma za afya ambazo hulazimika kuzifuata katika hospitali ya wilaya iliyoko Makunduchi, hasa huduma za uzazi za kujifungua lakini pindi hospitali hiyo itakapokamilika ujenzi, watapata unafuu mkubwa.

Boniface Robert anasema Kizimkazi ya sasa imeondokana na tatizo la maji safi na salama ambalo lilikuwa kubwa kabla ya Rais Samia kuingia madarakani.

"Kwa sasa Kizimkazi hatuna tena changamoto ya huduma ya maji safi na salama. Mradi mkubwa wa maji uliofikishwa kijijini hapo umebadilisha maisha yetu maana tulikuwa na changamoto kubwa lakini sasa tuna maji ya kutosha," anasema.

Neema hiyo ya maji, anasema haijawanufaisha wananchi wa Kizimkazi pekee bali hata wamiliki wa hoteli katika kijiji hicho ambacho hivi sasa kina hoteli nyingi za kitalii zenye hadhi tofauti.

"Mradi huu wa maji safi na salama ameuzindua mwenyewe Rais Dk, Samia mwaka jana. Sasa Kizimkazi ina maji ya kutosha. Kwa kweli Mama Samia amefanikiwa kuwatua ndoo kichwani wana Kizimkazi hasa wanawake ambao ndio watafutaji wakubwa wa maji," anasema.

**SHULE YA KISASA**

Kuhusu elimu, anasema Kizimkazi imepata shule ya kisasa ya ghorofa na kubainisha kwamba kabla ya uongozi wa Rais Samia, hakukuwa na shule ya ghorofa bali shule za kawaida zilizojengwa tangu wakati wa ukoloni.



Moja ya fukwe za Kizimkazi

"Hivi sasa Kizimkazi tuna shule nzuri za maandalizi, msingi na sekondari. Licha ya kujengwa shule hiyo ya ghorofa pia zile shule ambazo zilijengwa zamani zimefanyiwa ukarabati na kuongezwa madarasa. Sasa watoto wetu wanapata elimu katika mazingira mazuri," anasema Robert.

Anasema shule hizo zina vifaa vya kisasa zikiwamo maabara hali ambayo imeongeza ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa ya darasa la saba na kidato cha pili na hakuna mwanafunzi aliyepata alama sifuri.

**UTALII KIZIMKAZI**

Kuhusu sekta ya utalii, alisema Zanzibar imefunguka na Kizimkazi utalii umeimarika na kwa sasa kuna watalii wengi na kasi ya ujenzi wa hoteli na nyumba za kulala wageni imeongezeka.

"Hivi sasa uchumi wa mtu mmoja mmoja umeongezeka maana kuna kasi kubwa ya ujenzi wa nyumba za biashara kwa ajili ya kulaza wageni. Pia ajira kijijini hapa zimeongezeka kutokana na kasi ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha michezo na Barabara," anasema.

Pia anasema nyumba nyingi kijijini hapo zina umeme tofauti na ilivyokuwa awali kutokana na hali za kiuchumi za wananchi kuwa mbaya. Lakini sasa, anasema kuimarika kwa uchumi wao kunatokana na shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Hivi sasa ardhi Kizimkazi imekuwa na thamani kubwa bei za viwanja hazishikiki tofauti na miaka mitatu nyuma na sasa kuna ongezeko kubwa la watu," anasema.

Pia anasema filamu ya The Royol Tour ya Rais Samia imeleta manufaa makubwa kwa Zanzibar, ambapo sekta ya utalii imezidi kuimarika. Hivi sasa watalii wengi wanafurahi kufika Kizimkazi kijiji ambacho anatoka Rais Samia.

Sheha wa Kizimkazi Mkunguni, Mwachumu Shaka Ali, anasema Kizimkazi ya sasa iko mbele kimaendeleo na hivi karibuni wanawake wa kijiji hicho watajifungua katika hospitali inayojengwa kijijini hapo badala ya kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Makunduchi.

Anasema uongozi wa Rais Samia ni neema kwa Zanzibar nzima na si kwa wanakizimkazi pekee lakini wana Kizimkazi wanajivunia maendeleo ya kijiji chao ndani ya miaka mitatu ya uongozi wake.

**FEDHA ZA UVIKO-19**

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, anasema Rais Samia aliingia madarakani katika kipindi kigumu nchi ikiwa katika janga la UVIKO- 19 ambalo kwa kiasi kikubwa liliathiri na kuzorotesha mwenendo wa uchumi wa Tanzania katika sekta muhimu.

Anasema baada ya kushika madaraka, alifanya mazungumzo na taasisi zinazosimamia mwenendo wa fedha na ukuaji wa uchumi kwa ajili ya kufufua uchumi na kurudisha mzunguko halisi wa uchumi na fedha.

Mazungumzo hayo, anasema yalizaa matunda na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) lilikubali kuipa Tanzania mkopo nafuu wa Sh.Trilioni 1.3 kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO- 19.Anasema katika fedha hizo, Rais Samia aligawa mafungu serikali za Zanzibar na Muungano. Katika fedha hizo, anasema Zanzibar ilipata mgawo wa Sh. bilioni 230 kwa ajili ya kukabiliana na athari za ugonjwa huo katika maeneo ambayo yameathirika vibaya yakihusisha jamii moja kwa moja.

Mazrui anasema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, ilizigawanya fedha hizo katika maeneo tofauti muhimu kama afya, elimu na uchumi wa buluu.

Waziri huyo anasema katika sekta ya afya, serikali ilijenga hospitali 10 kwa kila wilaya Unguja na Pemba na hospitali moja ya mkoa ambayo iko Lumumba, Zanzibar.

Kwa mujibu wa Mazrui, katika fedha hizo, Wizara ya Afya ilipewa Sh. bilioni 39 na hivyo kuwezesha kujenga hospitali 11 za kisasa kwa kila wilaya ya Unguja na Pemba. Anasema hospitali hizo zimeanza kutoa huduma kwa wananchi hatua ambayo imelenga kufikisha huduma za wananchi hadi vijijini na kupunguza vifo vya kinamama na watoto.

**SEKTA YA ELIMU**

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, anasema katika sekta ya elimu, fedha za UVIKO- 19 zilitumika katika ujenzi wa shule 22 za ghorofa Unguja na Pemba zikiwamo shule mbili za elimu mjumuisho kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wenye ulemavu kujifunza kazi za vitendo.

Anabainisha kuwa sekta ya elimu ilipata mgawo wa Sh. bilioni 38 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya sekta ya elimu ikiwemo ujenzi wa shule mpya, ukarabati shule kongwe na kutengeneza madawati kwa ajili ya wanafunzi.

Alisema katika fedha hizo malengo ilikuwa kujenga shule 16 lakini wamepata mafanikio mazuri zaidi katika matumizi mazuri ya fedha hizo na kujenga jumla ya shule 25 za ghorofa ikiwemo za msingi na sekondari

**KAULI YA MWINYI**

Rais Mwinyi alimshukuru Rais Samia katika maboresho makubwa ya kiuchumi ikiwamo sekta ya fedha pamoja na ujenzi wa demokrasia.

Anasema uchumi wa Zanzibar umeimarika katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia katika baadhi ya sekta kupiga hatua kubwa ikiwamo uchumi wa buluu ambayo ni sehemu ya kipaumbele cha serikali ya Zanzibar.

Pia anasema kupatikana kwa fedha za UVIKO - 19 na kutumiwa vizuri katika eneo la uchumi wa buluu, sekta ya uvuvi imeimarika na kuchangia pato la taifa kwa asilimia 15 kutoka saba. Anasema hiyo inatokana na kuwawezesha wavuvi kupata vyombo vya kisasa na kuwawezesha kuingia katika maji marefu.

Anasema boti za uvuvi 530 zimegawiwa kwa wavuvi vikiwamo vifaa vya kisasa vitakavyowawezesha wavuvi kuwaonyesha wapi wapo samaki na kwenda kuwavua.

"Tumetumia Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kuwawezesha na kuwapatia wavuvi boti 530 sambamba na wakulima wa mwani boti 500 hatua ambayo imeleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika sekta hiyo na kuchangia pato la taifa kufikia asilimia 15," anasema.

Pia anasma sehemu kubwa ya fedha imepelekwa kwa wajasiriamali ikiwamo wa uchumi wa buluu, ujenzi wa viwanda vya kusarifu na kuongeza thamani katika zao la mwani ambacho kimejengwa Chamanangwe, Pemba kwa gharama ya Sh. bilioni 7.4.

Kiwanda kicho, anasema ni mkombozi kwa kuwa kitawawezesha wakulima wa mwani ambao kwa asilimia 80 ni wanawake, kuongeza juhudi ya uzalishaji kwa sababu uwezo wa kiwanda ni kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka.

Aidha, Dk. Mwinyi anasema serikali imejenga kiwanda cha kuchakata bidhaa za samaki aina ya dagaa ambacho zitaongeza thamani zao hilo ambalo huwajumuisha wajasiriamali wanawake.

Kuhusu sekta ya maji, anasema katika fedha hizo za UVIKO-19, serikali ilitenga Sh. bilioni 43 katika kutekeleza miradi ya upatikanaji maji safi na salama.

Fedha hizo, anasema zilitumika katika ujenzi wa matangi makubwa ya juu na chini pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji safi na salama ambayo mingi ilichakaa sambamba na kuimarisha vyanzo vya maji.

# Waziri apiga 'stop' uagizaji nondo nje

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema Tanzania inajitosheleza kwa nondo na mabati, hivyo hakuna haja tena kwa serikali na taasisi zake kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Pia ameziagiza taasisi zinazonunua bidhaa za ujenzi kutoka kwa wazalishaji wa ndani kuhakikisha wanalipwa kwa wakati ili wawekeze zaidi na kuongeza ajira nchini.

Alitoa agizo hilo jana Kisemvule, Mkuranga mkoani Pwani, alipotembelea kiwanda cha Lodhia Industries kuona uzalishaji na kusikiliza changamoto za mwekezaji huyo.

Kiwanda cha Lodhia kimewekeza Dola za Marekani milioni 120 kwenye uzalishaji wa nondo, mabati na bidhaa za plastiki na kwa mwezi kinazalisha tani 18,000 za nondo na matarajio ni kuzalisha tani 1,000,000 kwa mwaka.

"Tumeshajitosheleza kwa nondo na si kujitosheleza tu. Nimeshunudia kiwanda cha Lodhia wanatengeneza nondo zenye ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa. Kwa hiyo tununue vya kwetu tuachane na utegemezi wa kuagiza kutoka nje.

"Nnitoe rai kwa taasisi zinazopata zabuni za ujenzi wa miradi mbalimbali ya serikali lazima tuanze kutumia bidhaa zetu zinazozalishwa hapa nchini kwa sababu tumeshuhudia ubora kwa hiyo hatuwezi kuwa na visingizio," alisema

Prof. Mkumbo alisema moja ya malengo makubwa ya serikali ni kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi kulinda hazina ya fedha za kigeni na kwamba kiwanda cha Lodhia kimekuwa mkombozi kwenye uzalishaji wa shehena ya kutosha ya nondo zinazotumika katika miradi mbalimbali ya serikali.

Alisema kiwanda hicho kimepanuliwa na kuanza kutengeneza malighafi za kutengeneza misumari hatua ambayo alisema ni ya kupongezwa kwani itapunguza utegemezi wa kuagiza malighafi hiyo nje ya nchi.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukiagiza malighafi za kutengeneza misumari na mabati lakini wenzetu hawa wameshaanza kutengeneza malighafi hizi hii ni hatua kubwa sana ya kujivunia kwa maendeleo ya viwanda," alisema.

Alisema changamoto aliyobaini kwenye ziara yake ni kuwapo kwa uaagizaji wa nondo kutoka nje ya nchi licha ya kiwanda hicho na vingine kuzalisha bidhaa za kutosha na zenye viwango hivyo aliahidi kuchukua hatua.

Alisema kama miradi mikubwa kama ujenzi wa Reli ya Kisasa SGR na bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) imetumia bidhaa za ndani zikiwemo nondo hakuwezi kuwa na sababu ya kuendelea kuagiza kutoka nje.

"Kwa kweli kiwanda cha Lodhia kimeisaidia sana serikali kwenye eneo la kuacha utegemezi wa kuagiza bidhaa za nondo kutoka nje kwasababu bila wao tungetumia fedha nyingi za kigeni ndiyo maana naendelea kusisitiza tuthamini na tutumie vya kwetu," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Nasri, alisema uwekezaji uliofanywa na kiwanda hicho umekuwa na manufaa makubwa kwa wakazi wa Wilaya hiyo kiuchumi na ajira kwani vijana wengi wamekuwa wakinufaika nacho.

Alisema Lodhia ilianza na kiwanda kimoja cha kuzalisha nondo lakini kimeendelea kujipanua na kuongeza cha kuzalisha bidhaa za plastiki na sasa kinajenga kiwanda cha kuzalisha mabati ambacho kinatarajiwa kuanza uzalishaji mwezi Mei mwaka huu.

"Kiwanda cha mabati cha Lodhia kitakapoanza kazi hivi karibuni vijana wetu 600 watapata ajira hapa kwa hiyo tunashukuru mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo serikali yetu inaendelea kuyaweka na kuvutia wawekezaji," alisema

## Wanafamilia wauawa na mtu anayedaiwa ana tatizo la akili

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATU watatu wa familia moja akiwamo mtoto wa mwaka mmoja na miezi mitatu wakazi wa Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara wameuawa na mtu anayedaiwa kuwa na tatizo la afya ya akili.

Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, alisema tukio hilo lilitokea Machi 13, mwaka huu, saa 4:00 asubuhi katika Kitongoji cha Kwaona.

Katabazi alisema mtuhumiwa anaitwa Haika Daaki (42) ambaye aliwashambulia kwa panga watu wanne na watatu kati yao kupoteza maisha.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni ugomvi wa familia ambao aliuanzisha yeye (mtuhumiwa) na mke wake ambaye hakutajwa majina yake.

Akizungumzia tukio hilo, Neema John, alisema mtuhumiwa ana historia ya kuwa na tatizo la afya ya akili.

"Sisi tulisikia yowe tulipokwenda, tuliona mke wake ambaye alikuwa mjamzito ameshafariki dunia,"alisema John Alisema mtuhumiwa alikamatwa na kupelekwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Daniel Bura alisema mtuhumiwa alitaka kumnyonga mtoto wake ndipo mke alipoingilia na kuibuka ugomvi. Alisema mama wa mtuhumiwa aliingilia kati ugomvi huo na kuambulia kupigwa shavu na kuamua kukimbia.

Alisema mama yake alimpiga kisa alihoji ugomvi wao na familia yake. Jirani mwingine, Juma Abdul, alisema tukio la namna hiyo halijawahi kutokea kijijini hapo.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | MUGOO CONSTRUCTION CO. LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 52866 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 52865 | AFRED MUGOO MUNGWE | NYEGEZI MWANZA | 05/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 300-SNGLR, KIWANJA NAMBA 794 &796 KITALU 'A' CHAPWA TUNDUMA | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | CHAPWA TUNDUMA | 7/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | CESILIA PASCHAL MUSHI | NYUMBA | MAISHA STEVEN MUSHUNGUZI | MABIBO | 05/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | NYUMBA | KURUTHUMU ABDALLAH NYAMKO | NYAKATO -MWANZA | 26/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | LITTLEWOOD NURSERY AND PRIMARY SCHO | TOYOTA HIACE T362DMF | MARWA NTAGIRA NTAGIRA | KINYEREZI | 04/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | NYUMBA | STEPHANO CHACHA NYAMHANGA | MIYUJI - DODOMA | 05/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MUSTAFAH IDD GEKE | NYUMBA | MUSTAFAH IDD GEKE | MABWEPANDE | 05/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ANNA ULUWEKA MAMMBA | NYUMBA | MWANAHAMISI ZUBERI OMARY | MBEZI KWA MSUGURI | 06/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | EZRA YOTAM KIRAGI | NYUMBA | EZRA YOTHAM KIRAGI | NZASA A-CHARAMBE | 08/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | MBEZI LUIS-KIBANDA CHA MKAA | 06/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | CESILIA SAMWEL KWEKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA KUU | 26/03/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | VIWEGE MAJOHE | 08/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMRANI SADIKI MGALULA | NYUMBA | AMRANI SADIKI MGALULA | CHANIKA | 09/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JUMBE MHINA SALUM | NYUMBA | JUMBE MHINA SALUM | MKENGE-VIKAWE | 09/04/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0745707008/0715868000/0714939933/0754497396/0755337777/0759648448.**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba SC, Yanga jipangeni hakuna ushindi 'mdomoni'

**WAKATI** Tanzania ikiwa imeweka rekodi ya kutoa timu mbili katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, tayari rasmi wapinzani watakaocheza na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga katika hatua hiyo wamejulikana.

Simba yenyewe itacheza mechi ya robo fainali dhidi ya Waarabu wa Misri, Al Ahly wakati mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao watakutana na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Wawakilishi hao wawili wa Tanzania wote wataanzia nyumbani, Wekundu wa Msimbazi akimkaribisha Al Ahly Machi 29, mwaka huu na siku inayofuata Mamelodi Sundowns watakuwa ugenini dhidi ya Yanga, michezo yote ikifanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Timu zote nane zilizofika hatua hiyo ni kubwa, na kwa maana hiyo, hakuna timu ambayo inatakiwa kuingia uwanjani kinyonge, kufika hatua hiyo kunamaanisha kila klabu ilijiandaa vyema kupambana katika msimu huu.

Licha ya baadhi ya makocha kukosa wachezaji iliyowahitaji wakati wa usajili wa dirisha dogo, usajili uliokuwa na malengo ya kuviongezea nguvu vikosi vyao, bado suala la ukubwa liko pale pale, hakuna klabu ndogo inafika hatua ya robo fainali.

Simba na Yanga zinatakiwa kujipanga na kujiimarisha vyema kuhakikisha wanafanya vizuri na wanasonga mbele katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka kwa kuandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka la Afrika (CAF).

Vigogo hao wa soka nchini wanatakiwa wawaonyeshe mashabiki wa soka ndani na nje ya Afrika wao wamefika hapo kutokana na ubora waliokuwa nao na si kubahatisha, walipambana na kuwazidi waliokutana nao na hatimaye kutinga robo fainali.

Katika dunia ya sasa, soka ni mchezo wa kuwekeza, Simba na Yanga zimewekeza kwa kusajili wachezaji kutoka mataifa mbalimbali pamoja na makocha wa kigeni, hii inaonyesha wako tayari kupambana na kufikia ubora wa hao wanaoitwa wakubwa ambao wameshawahi kubeba ubingwa wa Afrika.

Huu ni wakati wa viongozi, makocha na wachezaji kila mmoja kujipanga kutekeleza vyema majukumu yake ili kufikia malengo ya kufanya vizuri na hatimaye kucheza hatua ya nusu fainali ambayo kwa Tanzania itakuwa ni habari nyingine kubwa.

Kama ambavyo, Simba na Yanga zimempa heshima Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwa kiongozi pekee wa nchi mwenye timu mbili katika hatua hiyo, wanatakiwa kufahamu wana kazi kubwa ya kupeperusha vizuri zaidi bendera ya Tanzania katika michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu.


Kama ambavyo baada ya kumalizika kwa fainali za Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita, tulishuhudia aliyekuwa straika wa Yanga, Fiston Mayele, akinunuliwa na Pyramids ya Misri kwa dau kubwa huku Kocha wao, Nasreddin Nabi akiondoka, pia huu ni wakati mwingine kwa nyota wa Simba na Yanga kufahamu wanaingia 'sokoni' na wanachotakiwa ni kujituma na kuonyesha viwango vya juu.

Ni wazi mechi zote za hatua ya robo fainali zinafuatiliwa na makocha na mawakala mbalimbali, huu ndio wakati wa wachezaji walioko katika klabu hizo mbili kuzipigania bendera za klabu zao lakini kwa maana nyingine na muhimu 'kujiuza' wao wenyewe.

Hakuna kinachoshindikana katika dunia ya sasa, Simba na Yanga huu ndio wakati wenu muhimu wa kuwafunga na kuwaondoa Al Ahly na Mamelodi Sundowns katika mashindano hayo ya CAF, kuanza vizuri ni kujiweka katika mazingira chanya, ingawa hata ugenini pia matokeo mazuri hupatikana.

Kitu kingine muhimu ni kwa mashabiki kuacha tabia ya kuwashangilia wageni kwa sababu kuendelea kufanya hivyo ni sawa na kulihujumu taifa lako, umefika wakati neno ushirikiano na umoja wa kweli kati ya watani wa jadi unahitajika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Simba malizeni tatizo la fiziki, itawasaidia Afrika

Na Adam Fungamwango

**SIKU** chache tu baada ya beki wa zamani wa Simba na Taifa Stars, Mtemi Ramadhani, kutoa masikitiko yake kuhusiana na wachezaji wa timu hiyo kutokuwa na fiziki na pumzi za kutosha, jambo hilo limejionyesha dhahiri katika mechi mbili za Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union na Singida Fountain Gate.

Ni mechi ambazo Simba imepata ushindi, lakini ulikuwa ushindi mgumu kutokana na ilifika wakati wachezaji wake walikata 'upepo' na kuanza kutafutana uwanjani.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba huombea mechi iishe wakati timu yao inapoongoza kwa sababu dakika za lala salama hushambuliwa sana, ukiondoa mechi moja tu ile ya hatua ya raundi ya sita ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilipocheza dhidi ya Jwaneng Galaxy na kuvuna ushindi mnono wa mabao 6-0.

Ni mechi hiyo tu ndiyo Wanasimba walionekana 'kuinjoi' wakiombea mpira usimalizike kutokana na kushuhudia timu yao ikitawala mechi hadi dakika za mwisho. Hiyo ni moja kati ya mechi chache walizofanya vyema msimu huu.

Sitaki kurudi nyuma sana, nianze kwenye mechi dhidi ya Coastal Union iliyopigwa Machi 9, mwaka huu Simba ilishinda mabao 2-1, ilionekana kutawala sana kipindi cha kwanza, lakini cha pili ilihangaika, kabla ya kupata goli la pili kutokana na uweza binafsi wa, Willy Onana.

Baada ya hapo timu ilionekana kukaa zaidi nyuma ili kulinda bao la pili walilopata badala ya kushambulia kitu ambacho si cha kawaida kwa timu kubwa kama hiyo dhidi ya kikosi cha Coastal Union.

Ukweli wachezaji wao wengi walionekana kuchoka au kwa lugha nyingine waliishiwa pumzi.

Mechi hiyo ikafanana kabisa na ile iliyochezwa Jumanne iliyopita dhidi ya Singida Fountain Gate waliyoshinda mabao 3-1, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ambapo ilipata mabao yake yote kipindi cha kwanza na kushindwa kuongeza hata goli moja kipindi cha pili licha ya kutengeneza nafasi nyingi.

Kipindi cha pili ilikamatwa na kuonekana kuchoka kabisa. Hili ni tatizo kubwa la Simba ya sasa, ambapo Mtemi linamsikitisha.

Kutokuwa na utimamu wa mwili kunasababisha wachezaji wacheze kigoigoi mno kama wapo mazoezini.

Na hii imenekana kama imeanza kuzoeleka kwa timu za Tanzania, makocha wao wameshatambua na ili kuwabana Simba ni kucheza kwa kutumia nguvu kwa sababu wachezaji wao hawapendi mapambano na mmoja kwa moja katika kugombea mpira, na mara nyingi hushindwa.

Hili sijalisema kwa wawakilishi wengine wa Tanzania katika mechi za kimataifa, Yanga kwa sababu hawana tatizo hilo.

Yanga wana fiziki na pumzi na ukitaka kuthibitisha mabao yao mengi huyafunga kipindi cha pili, na hucheza kwa kasi hadi dakika za mwisho. Hii inathibitisha wako timamu, kitu pekee ambacho kinaweza kuwaangusha kwenye mechi dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini labda ni mbinu za kiufundi na viwango vya wachezaji.

Simba kama inataka ushindi mnono dhidi ya Al Ahly ni lazima watengenezewe fiziki hata ya muda mfupi ili kuwamudu Waarabu hao, inatakiwa ipate ushindi mnono nyumbani, tena bila kuruhusu bao lolote kama ambayo huwa inafanya.

Pili pumzi na fiziki iongezeke tena mara dufu inapokwenda kucheza ugenini Cairo, huko ndiko itakuwa na kazi ngumu sana ya kuzuia mashambulizi mfululizo na hasa kama itakuwa imeshinda kwa kishindo nchini.

Hakuna timu inayoweza kuizuia Al Ahly nyumbani kwao mbele ya mashabiki wao wanaohanikiza jukwaani ikiwa inahitaji mabao, kama haitokuwa na wachezaji wenye utimamu wa mwili na pumzi, ambavyo vyote hivyo vinasababisha wachezaji kuweza kukimbia eneo kubwa la uwanja na kupambana.

Ili kuitoa Al Ahly haitakiwi tu timu iwe na wachezaji wazuri, bora na wenye vipaji, hivi nilivyovianisha pia vinatakiwa viongozeke kama Simba inataka kweli kwenda nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Wananchi wahofu uhaba wa mvua

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wakulima mkoani Rukwa wamekumbwa na hofu baada ya hali ya hewa kubadilika na kusababisha mvua kusimama kunyesha huku joto likiwa kali isivyo kawaida.

Wamesema hali hiyo inaweza kuathiri mazao hususan mahindi ambayo yamefikia hatua ya kubeba hivi sasa.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii kwa nyakati tofauti, wakulima hao walisema hivi sasa mvua zimesimama wakati mahindi yamefikia hatua ya kubeba na ni muda ambao yanahitajika maji mengi ili punje zijae vizuri lakini hali imekuwa tofauti ni wiki sasa imepita bila mvua kunyesha.

Mmoja wa wakulima hao, Atman Macheta, alisema hali hiyo imekuwa ghafla na kama itaendelea hivi kwa muda wa mwezi mzima, huenda ikaondoa matarajio ya wakulima kufanya vizuri katika mavuno ya mahindi.

Alisema hali hiyo imesababisha hofu kwa baadhi ya wakulima kutokana na baadhi yao kukopa fedha katika taasisi mbalimbali na watu binafsi na kununua mbolea, mbegu na viwatilifu na sasa wanahofia namna watakavyozirejesha.

Naye Pauline Kaswaya alisema hivi sasa jua limekuwa kali na mahindi yameanza kuonesha dalili za kunyauka na pepo zikivuma hali ambayo inaonyesha kuwa hakuna mvua, hivyo kuzidisha hofu kwa wakulima ambao wamefanya uwekezaji katika kilimo.

Alisema kilichopo sasa ni kumwomba Mwenyezi Mungu katika kipindi hiki cha mfungo wa Kwaresma na Ramadhan ili alete mvua na mahindi yabebe vizuri na wakulima wapate tija kwa kuwa kilimo ndilo tegemeo lao.

Felix Kibona ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Mkoa wa Rukwa, aliwataka wakulima kutokuwa na hofu kwa kuwa mvua bado zipo licha ya kwamba zimepungua na zinaelekea mwishoni.

Alisema kuwa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa Oktoba, mwaka jana, ulionyesha kuwa mvua itakuwa katika awamu mbili, ya kwanza mvua nyingi itanyesha kuanzia Novemba, mwaka jana, hadi Februari, mwaka huu, halafu itasimama na kisha kunyesha awamu ya pili katikati ya mwezi huu hadi mwezi ujao.

Kibona aliwasihi wakulima mkoani Ruka kuwa mvua hizi za mwishoni walime mazao kama maharage na alizeti ili wazitumie vizuri kwa kuwa zitakuwa na manufaa makubwa iwapo watazingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo. Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, Machi 11, mwaka huu, kupitia mtandao wake wa X, aliwataka wakulima kulima alizeti kwa kutumia mbegu ya kisasa katika mvua hizi za mwisho kwa kuwa mbegu ya ruzuku inapatikana kwa mawakala.

Pia aliiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kama kuna mkulima alimaliza sehemu yake ya ununuzi wa mbolea ya ruzuku na anataka alime tena katika mvua za mwisho, mfumo usifungwe ili akanunue tena mbolea na arudi shambani kwa mara nyingine.

# Wataka mabadiliko ya sera vikwazo vya bidhaa mipakani

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Shirika la Liberty Spark, Evance Exaud, amesema uwapo wa mabadiliko ya sera yatasaidia watanzania kuingiza na kuuza biashara mbalimbali bila kukutana na vikwazo katika mipaka.

Aliyasema hayo juzi Dar es Salaam katika mkutano wa majadiliano ya utafiti wa awamu ya pili ya Mradi wa Ujirani Mwema uliowaunganisha wadau mbalimbali ambao wanahusika na biashara ya mipakani.

Exaud alisema endapo serikali ikifanya mabadiliko ya kisera itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uchumi ndani ya nchi na watu kupata taarifa sahihi.

Alisema mradi wa ujirani mwema awamu ya pili, unalenga katika kuangalia matatizo au changamoto ambazo wafanyabiashara kutoka nchi moja au nyingine wanazozipata hususani katika biashara za mipakani katika kilimo, viwanda na madini.

"Mradi unataka kuona Tanzania inafanyaje biashara za mipakani na nchi jirani ili kurahisisha biashara zao, licha ya uwapo wa changamoto mbalimbali ikiwamo utumiaji wa muda mrefu kutuma mizigo au uingizaji wa mizigo, masuala ya kikodi pamoja na malipo kutokuwa sawa kisheria.

"Awamu ya kwanza ya mradi huu tuliangalia changamoto hizo na ndio maana awamu ya pili tumeweza kuangalia upande wa kilimo, madini na viwanda na kuona kuna haja ya kuangalia masuala ya kikodi," alisema. Exaud alisema kilimo, viwanda na madini ni sekta zinazochangia asilimia 50 ya pato la taifa huku asilimia 40 ya watanzania wakijikita katika kilimo, hivyo sekta hizo zimekuwa ni sehemu ya kuchochea uchumi wa nchi.

Alisema ili sekta hizo ziweze kukua ni lazima watanzania wapate masoko ya nje na kuuza pasiwapo na vikwazo vyovyote vinavyozuia mfanyabiashara kushindwa kufanya biashara kwa nchi jirani kama Kenya, Uganda na Rwanda.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC), Hamad Hamad, alisema vikwazo vya kisera na kikodi vinatakiwa kuondolewa ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara kufanya biashara bila vikwazo.

"Tunatakiwa kuongeza hamasa ya upelekeji wa bidhaa nje ya Tanzania, kwani tunapoingiza zaidi biashara nchini pato tunalopata linakuwa dogo kuliko tunapotoa zaidi biashara nje ya nchi tunakuwa tunaingiza fedha nyingi zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa Utafiti na Elimu Shirika la Liberty, Michael Kihande, alisema wamekuwa wakiwashauri watendaji kuhusu kubadilisha sheria, taratibu au sera zilizopo ambazo wafanyabiashara wanazitumia ili kurahisisha watanzania kupata fursa za nje ya nchi kufanya bi-



Mtaalamu wa afya, Dk. Mariam Yondu akizungumza kwenye hitimisho la mradi wa MomCare wa shirika la PharmAccess, katika mji mdogo wa Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wadau waibuka na maazimio makuzi watoto

**Na Sabato Kasika**

KONGAMANO la siku nne kimataifa la malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, lilimalizika juzi jijini Dar es Salaam huku washiriki wakitoka na maazimio ya kwenda kufanyia kazi katika nchi zao.

Maazimio hayo yalisomwa na Ofisa Mkuu, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambaye anashughulikia Jinsia na Maendeleo ya Jamii, Generose Minani.

Alisema wadau hawana budi kushirikiana na serikali za nchi zao kusimamia malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Pia alisema wadau hao kwa pamoja wameazimia kuhimiza uwekezaji zaidi katika elimu malezi na lishe kwa kuwa watoto wengi bado wanakumbana na maradhi mbalimbali kutokana na lishe duni kwenye ukanda wa Mashariki mwa Afrika.

"Tumeazimia pia kwenda kusimamia usawa wa kijinsia, kwa pamoja tuchukue hatua kuimarisha vipaumbele na ajenda za nchi za ukanda wetu kwa kushirikiana na wadau wote," alisema Minani.

Aidha, katika azimio lingine ni mawaziri kuwajibika kwa uwazi katika serikali zao na kuhamasisha utoaji wa elimu ya malezi na makuzi.

"Vilevile, uwapo mpango wa maalum wa kutambua usalama wa mtoto, kuhamasisha utafiti na uvumbuzi kwenye ukanda wetu ili kuimarisha ulinzi wa mtoto, aliongeza.

Aidha, alisema washiriki hao wameazimia kujikita katika kuchambua masuala mbalimbali ya makuzi ya mtoto kwenye ukanda huo ili kila taifa liwe na mikakati maalum kulingana na mazingira yake.

Akifunga kongamano hilo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdul Gullamhussein, aliwataka washiriki hao kwenda kutumia katika zao ujuzi walioupata ili kuwa na matokeo chanya ya malezi na makuzi ya watoto.

Naibu Waziri huyo pia aliwataka wadau wa maendeleo ya mtoto katika nchi za ukanda huo, kuunga mkono juhudi za serikali zao katika kusimamia malezi na makuzi ya mtoto ili kuandaa kizazi bora cha baadaye.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju, aliwataka washiriki kuwa mabalozi malezi na makuzi ya watoto katika nchi zao.

"Washiriki wa kongamano nendeni mkawekeze katika malezi na makuzi ya watoto kwa kufuata mila na desturi za kiafrika bila kuchanganywa mila za kigeni kuwa na mataifa imara ambayo hayawezi kuparaganyika," alisema Mpanju.

Wakati akifungua kongamano hilo Jumatatu iliyopita, Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema bado kuna tatizo la malezi na makuzi ya mtoto katika nchi za Afrika.

Alisema utafiti mbalimbali uliofanyika katika nchi za Afrika, ulibaini kuwa uwekezaji katika malezi makuzi ya watoto wadogo bado mdogo.

Kutokana na hali hiyo, akazitaka serikali za nchi ambazo zilikuwa na wawakilishi katika kongamano hilo kutenga bajeti, kwa ajili jambo hilo, ili kulinda taifa lijalo.

Alifafanua kuwa elimu ya malezi na ya lishe bora inatakiwa kuanzia ngazi ya familia, kwa wazazi na walezi kufanya sehemu yao kwa manufaa ya familia, jamii na taifa kwa ujumla.

# CBE yapewa mchongo ubunifu soko la ajira

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imekitaka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kuweka mikakati ya kujiimarisha kiteknolojia, uvumbuzi na ubunifu ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira ambayo yanakwenda kwa kasi.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, wakati wa mjadala wa Dira ya Maendeleo ya miaka 50 ya chuo hicho itakayotekelezwa hadi mwaka 2074.

Alisema chuo hicho kinapaswa kutoa elimu ambayo itakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi kwa kuwa na wahitimu wenye weledi wa kutosha kupokelewa na waajiri popote watakapokwenda.

Alisema sekta ya biashara ni kiungo muhimu katika kukuza biashara nchini na kukuza uchumi hivyo sekta hiyo inapaswa kutoa elimu bora kwani ndio msingi wa maendeleo ya uchumi nay a kijamii.

Alikipongeza chuo hicho kwa kuendelea kufanya mageuzi yanayoendana wakati na teknolojia katika fani ya biashara na juhudi zake za kujenga uwezo wa kitaaluma na kiufundi kwa wanafunzi wa chuo hicho.

"Dira ya miaka 50 ya chuo cha CBE ambayo imeandaliwa kwa umahiri mkubwa na kwa kushirikisha wadau mbalimbali ni hatua muhimu katika kuhakikisha chuo hiki kinabaki kuwa imara katika kutoaelimu bora na kusaidia ukuaji wa biashara," alisema.

Dk. Abndallah alisema ni matumaini ya serikali kuwa iwapo dira hiyo itatekelezwa kwa ufasaha itasaidia kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya biashara na kwenye jamii kwa ujumla.

Alisema chuo hicho kinapaswa kuwa tayari kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika taasisiz a elimu ili kiwe na uwezo wa kubailika kwa haraka kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, alisema katika kampasi zake zote chuo hicho katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Dodoma kina wanafunzi 19,000 na kwamba wamekuwa wakijitahidi kutoa elimu kwa vitendo zaidi. Aidha, alisema katika kutekelez dira yake ya miaka 50 walishaanza kufanya mageuzi ya kutoa nelimu kwa vitendo ambapo walifanikiwa kuanzisha program za uanagenzi ambapo wanafunzi husoma wakiwa wanafanyakazi kwa vitendo.

"Na napendaa kutoa taarifa kuwa tumeshapata ithibati ya programu za uanagenzi na mwaka huu tutaanza na kozi za benki na metrolojia ambapo watakuwa nusu shuleni na nusu watakuwa kazini," alisema.

Prof. Lwoga alisema kwenye kozi ya metrolojia watashirikisha na Wakala wa Vipimo (WMA), ambapo wanafunzi watakuwa darasani kwa muda na watakwenda kufanyakazi.

Alisema CBE ilishaanzisha program atamizi kwa wanafunzi wenye ndoto ya kuanzisha biashara kupelekwa mawazo yao ambayo huboreshwa na kupewa mafunzo ambayo hatimaye huwawezesha kufanya biashara hizo.

"Tumeshaanza sasa ni miaka miwili na wanafunzi wengi wameshajitokeza kusajili biashara na kampuni zao wakiwa bado chuoni na katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia tumeshaanzisha masomo ya mtandao," alisema.

Prof. Lwoga alisema kwa kuanza wameanza kutoa Shahada sita za Uzamili kwa njia ya mtandao na kwamba wataongeza kozi ya biashara ya kimataifa na kozi ya ununuzi na ugavi.

Alisema dira yao ya miaka 50 inawakilisha maono ya wanafunzi na wadau wote wa chuo hicho kwani chuo kimejitahidi kushirikisha maoni ya watu wengi wakati wa kuandaa dira hiyo.

Alisema miongoni mwa sababu zilizochochea chuo hicho kuandaa dira hiyo ni mabadiliko ya teknolojia kama akili bandia, roboti na utandawazi.



Mkurugenzi wa Kiwanda cha Lodhia Industries, Sailesh Pandit (mwenye kofia ya kijani), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi wa Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), Leodegar Tenga (wa tatu kushoto), Makamu Mwenyekiti wa shirikisho hilo, Samuel Nyantahe (wa pili kushoto) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Manoj Gopi (kushoto), walipotembelea kiwandani hapo, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ujenzi daraja la JPM wafikia asilimia 85

**Na Remmy Moka,** SAUT

UJENZI wa Daraja la Kigongo-Busisi, maarufu kama Daraja la JPM, umefika asilimia 85 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, mwaka huu na kuunganisha barabara kuu ya Usagara-Sengerema kuvuka Ziwa Victoria.

Taarifa ya ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa kilometa 3.2 pamoja na barabara unganishi ya kilometa 1.66, ilitolewa jana mkoani Mwanza katika ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyofika kukagua maendeleo ya mradi huo na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mhandisi Doroth Mtenga.

Alisema mradi huo umekuwa ukitumika kama darasa la mafunzo kwa wanafunzi na wataalamu wa uhandisi wa ndani ili kupata uzoefu wa kusimamia na kujenga madaraja mengine kama hayo hapa nchini.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Kakoso, alisema kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi huo na kuiagiza Wizara ya Ujenzi kuhakikisha inamsimamia mkandarasi kutoa fedha zitakazoisaidia jamii inayozunguka mradi huo ambazo zitakuwa kielelezo kwa wananchi wa wilaya za Sengerema na Misungwi. Aidha, Kakoso alitaka wizara hiyo kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama katika daraja hilo ambalo linatokana na kodi za wananchi ili lidumu kwa miaka 100 kama ilivyokusudiwa.

Naye Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema mpaka sasa Sh. bilioni 441.3 zimetolewa kwa ajili ya kumlipa mkandarasi anayetekeleza mradi huo.

"Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa kila hati za mkandarasi zinazowasilishwa na zimekuwa zikilipwa kwa wakati ili asikwame kutokana na kukosekana kwa fedha kwa namna yoyote," alisema Bashungwa.

## Mradi kusaidia wasichana umri balehe waibuliwa

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la 'Jukwaa la Utu wa Mtoto' (CDF) kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni jana wamezindua mradi wa kuwasaidia wasichana wenye umri wa balehe kufahamu haki zao na namna ya kujilinda na virusi vya Ukimwi pamoja na matumizi sahihi ya dawa za kufifisha makali ya virusi hivyo 'ARV'.

Uzinduzi huo ulifanywa na Mganga Mkuu wa Manispaa hiyo, Dk. Ezra Ngeleza na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Koshuma Mtegeti.

Akizungumza kabla ya uzinduzi huo, Mtegeti alisema lengo la mradi huo ni kuona wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 wanakuwa na uwelewa wa haki zao za msingi, lakini pia wanafahamu kuhusu virusi vya ukimwi, namna bora ya kujilinda lakini pia namna ya kutumia kwa usahihi dawa za ARV.

"Mradi huu unakuja kutokana na hali ya ukatiri kwa watoto wa kike, pamoja na uwelewa mdogo wa masuala ya HIV na haki za mtoto wa kike, tutaufanya kwa kipindi cha miezi tisa na tutajikita kwenye kata za Mwenge, Makumbusho, Magomeni na Tandale.

"Ambapo kwa asilimia kubwa tutawalenga wasichana walioko kwenye mazingira hatarishi, lengo ni kuona uwelewa wa masuala ya haki ya mtoto wa kike na msicha kwa ujumla wanazifahamu, wanakuwa na uwelewa wa namna ya kujilinda," alisema Mtegeti.

Aidha, alisema kuwa katika mradi huo watatumia waelimisha rika 20 ambao watapewa mafunzo na kuwezeshwa hili wawafikie wasichana 200 wa manispaa hiyo kuwapa elimu hiyo.

"Tunatarajia kuwafikia wasichana 200 katika kata hizo, tunaamini baada ya mradi huu, kutakuwa na uwelewa mkubwa kwa wasichana juu ya mambo hayo tunayoenda kuyafanyia kazi kwenye mradi huu," alisema Mtegeti.

Alisema mradi huo wameutekeleza Mkoa wa Mara na kupata mafanikio makubwa kwa kuwapa wasichana elimu, pamoja na kupunguza hali ya ukatiri kwa wasichana na watoto wa kike.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kinondoni, Dk. Ngeleza, alisema mkradi huo umefika katika manispaa hiyo kwa wakati kutokana na elimu ndogo juu ya masuala ya haki za watoto wa wasichana.

Alisema kuwa hali ilivyosasa bila kuwa na jitihada za kutoa elimu na kuelmisha, taifa halitafikia malengo ya millenia ya kufikia maambukizi sifuri ya VVU ifikapo mwaka 2030 hivyo juhudi za dhati zinahitajika.

"Nawaomba pia Jukwaa hili liangalie uwezekano wa kupanua wigo wa wasichana wengi wa manispaa yetu kupata elimu hii, tusiishie kwenye kata hizi nne bali muangalie uwezekanowa kwenda na kata za pembezoni," alisema Dk. Ngeleza.

Aidha, alisema katika utoaji huo wa elimu vijana wa kiume na wanaume wanapaswa kupewa nafasi kwa kuwa wana mchango mkubwa katika kuwasaidia wasichana kufahamu haki zao.

# Walia utitiri kampuni bubu ulinzi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAMILIKI wa kampuni binafsi za ulinzi wameiomba serikali kuwasaidia kuwa na sheria itakayowasimamia ili kuondoa kampuni bubu ambazo zimekuwa zikichukua kazi kwa bei ndogo kutokana na kutolipa kodi za serikali.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Kampuni Binafsi za Ulinzi Tanzania (UKUTA), Abel Ndedwa, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa nne uliofanyika jijini hapa jana.

Ndedwa alisema anaomba serikali kuwasaidia kutungwa kwa sheria ya makampuni ya ulinzi nchini ili kuondoa kampuni bubu ambazo zimekuwa zikiongezeka kila siku.

"Kuna kampuni nyingi bubu za ulinzi hapa nchini, hivyo tunaiomba serikali kutunga sheria ambayo itaondoa tatizo hili ambalo linasababishwa na kutokuwepo kwa sheria hizo za kuwabana "alisema.

Alisema kwa sasa kampuni hizo zinasajiliwa na kufanya kazi chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kusimamiwa na Jeshi la Polisi.

Kadhalika, alisema uwapo wa kampuni hizo bubu za ulinzi kunaikosesha serikali mapato kutokana na kutolipa kodi mbalimbali.

Alisema kutungwa kwa sheria maalumu ya kampuni hizo pia itasaidia kuwafuatilia wanaokiuka masharti ya kuanzisha kampuni binafsi za uliunzi bila kusajili na itasaidia kutamka adhabu kwa watakaovunja sheria hizo.

Pia, alisema baadhi ya walinzi wa kampuni bubu wamekuwa wakishiriki vitendo vya uhalifu maeneo yao ya kazi kutokana na kuajiriwa bila kufuata taratibu zilizopo za kuajiri walinzi.

Makamu Mwenyekiti wa UKUTA, Janeth Lushuri, aliwaomba wenye kampuni za ulinzi nchini kuwapanga walinzi wa kike zamu za mchana ili usiku wakahudumie familia zao. Lushuri alisema askari wote wanahaki ya kufanyakazi muda wowote lakini aliomba walinzi hao wa kike kupangiwa malindo ya mchana

"Mimi binafsi katika kampuni yangu ya ulinzi nimeshapata malalamiko ya kuvunjika kwa ndoa za baadhi ya askari wa kike kutokana na kufanya kazi usiku hivyo nawaomba kuwatazama kipekee askari hao wa kike ili wahudumie watoto na familia zao wakati wa usiku "alisema.

Mwenyekiti wa UKUTA, Amani Mbijima, alisema kampuni binafsi za ulinzi zinasaidia kutoa ajira nchini na kwa sasa ziko 1,648 ambazo kila moja imeajiri zaidi ya wafanyakazi 100.

Mkurungenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ulizi ya Jito kutoka mkoani Geita, Daniel Machombe, alisema wanakabiliwa na kodi nyingi ambazo zimesababisha wengi kufunga kampuni zao.

# 'Vijana msitumike kwa mwamvuli wa ahadi ajira'

**Na Mwandishi Wetu,**
IRINGA.

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM ya Taifa, Mohammed Ali Kawaida ametoa angalizo kwa vijana nchini kuacha kutumika kwa mwamvuli wa ahadi za ajira kwa kuwa tatizo la ajira ni la dunia nzima na si Tanzania pekee.

Kawaida na ambaye pia ni Mlezi wa UVCCM vyuo na vyuo vikuu nchini, alitoa angalizo hilo juzi mkoani Iringa wakati akizungumza na viongozi wa UVCCM Seneti ya Vyuo na Vyuo Vikuu katika ofisi ya CCM Mkoa wa Iringa.

Alikemea vitendo vya wanasiasa kutumia vijana kusukuma ajenda zao na kujinufaisha kupitia kundi hilo.

"Vijana amkeni, msikubali kutumika kusukuma ajenda za watu ili wafanikishe mambo yao kwa maslahi yao binafsi. Serikali yenu ya awamu ya sita inayoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuchukua jitihada mbalimbali kuhakikisha vijana mnapata mikopo ili mjikwamue kiuchumi," alisema Kawaida.

Kiongozi huyo wa CCM alielekeza viongozi wenzake wa UVCCM kuhamasisha vijana wote wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura na kutumia haki yao ya msingi kupiga kura kuchagua viongozi wanaowataka ambao watawasaidia kutatua changamoto zinazowakabili.

Kawaida alisisitiza ushiriki wa vijana katika uchaguzi, akisema UVCCM itahakikisha inaunga mkono vijana wote watakaojitokeza kugombea nafasi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Wito wangu kwa vijana, jitokezeni kugombea katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu. Gombeeni nafasi za udiwani na ubunge, na sisi tutawaunga mkono ili tupate uwakilishi wa vijana ngazi ya kata na bungeni," alisema.

Kawaida yuko katika ziara ya siku tatu mkoani Iringa ambayo pamoja na mambo mengine, jana alitarajiwa kufungua Mkutano Mkuu wa UVCCM Vyuo na Vyuo Vikuu uliopangwa kufanyika kitaifa Iringa.



Mjumbe wa Halmashuri Kuu ya CCM Wilaya Dodoma, Christina Kamunya akizungumza na viongozi wa kata na matawi wa chama hicho, katika kikao cha kumtambulisha mlezi wa CCM Kata ya Kizota, wilayani humo jana.Wengine ni Katibu wa CCM kata hiyo, Yuda Makalangu (kushoto), (wa pili kushoto) ni Mwenyekiti wa Chama wa kata hiyo, Habib Sinkala na (kulia) ni Diwani wa kata hiyo, Jamal Ngalya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Anwani za makazi ajenda vikao kata

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imedhamiria suala la anwani ya makazi kuwa ajenda muhimu na endelevu ili kurahisisha usimamizi na uhakiki wa taarifa za anuani za makazi.

Kutokana na umuhimu huo, watendaji wa vijiji,kata na mitaa katika halmashuri zote nchini wametakiwa kulizungumzia kwenye vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata (WDC).

Mtaalamu wa Mfumo wa Anwani za Makazi kutoka wizara hiyo, Innocent Jacob, alisema hayo jana wakati wa mafunzo ya siku mbili ya Uhakiki Anwani za Makazi katika Mfumo wa Kidigitali (NaPA).

Mafunzo hayo yanatolewa kwa watendaji wa kata, vijiji na mitaa na wenyeviti wa Mitaa na vijiji wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida kwa ajili ya uhakiki wa anwani za makazi.

Jacob alisema anwani za makazi ni muhimu sana kwasababu zinasaidia ulinzi na usalama,kutoa huduma kwa wakazi na pia inasaidia biashara mtandao kupitia mfumo wa kidigitali (NaPA).

"Anwani za makazi ni miundombinu ya mawasiliano inayorahisisha utambuzi wa mtu alipo au mtu stahiki alipo aidha mahali pa kazi biashara au ofisi aweze kupata huduma kwa urahisi," alisema.

Jacob alisema mfunzo kwa viongozi hao yanatolewa ili kuwawezesha kwenda kuhakiki taarifa za wakazi wao katika maeneo yao ya kiutawala ambapo zoezi hili la uhakiki wa anwani za makazi katika awamu ya kwanza linafanyika katika Manispaa za Singida, Iringa na Kigoma na baadaye litafanyika nchi nzima.

"Tunafahamu mfano katika Manispaa ya Singida kuna kata18 na mitaa 72 kwa hiyo tunataka kuona wakazi wanahakikiwa taarifa zao kwani wapo ambao baadhi ya taarifa hazikuingizwa kwenye mfumo kipindi zoezi hilo lilipofanyika,"alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Adrianus Kalekezi, akifungua mafunzo hayo alisema uwepo wa anwani za makazi utakuwa msaada mkubwa kwa jamii kama ilivyo kwa nchi zilizoendelea.

"Hizi anwani za makazi ni maagizo kutoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwamba nchi nzima twende kwenye Anwani za Makazi na zoezi hili lilianza tangu huko nyuma.

"Kuwapo wa anwani za makazi kuna faida kubwa jambo ambalo litakuwa msaada kwa wakazi na nchi yetu kwa ujumla kama ambavyo Ulaya wamekuwa na utaratibu huu ambao umekuwa rafiki.

Hapa tunapewa elimu zaidi, ili kwenda katika kata, mitaa na vijiji vyetu kuona mambo yanaenda sawa kwa kuwa na anwani za makazi, lakini pia mafunzo haya yatajenga uelewa hasa katika Mfumo wa kidigitali (NaPA)," alisema.



# Mitandao yatumika usafirishaji wanyamapori

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa** BAGAMOYO

MITANDAO ya Kijamii imetajwa kutumiwa na majangili katika kufanya biashara ya usafirishaji wa wanyamapori na viumbe hai kinyume cha sheria.

Ofisa Wanyamapori kutoka Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA) Kitengo cha Uchunguzi wa Makosa ya Wanyamapori, Tryphone Kanini, alisema hayo jana wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari za mazingira yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) yaliyofanyika mjini hapa.

Alisema katika kudhibiti makosa ya wanyamapori, wamebaini kuwa kuna baadhi ya makosa ya yanatendwa kupitia mitandao ya kijamii.

Kutokana na kubaini hilo, alisema mamlaka imekamata baadhi ya watuhumiwa na jitihada mbalimbali zinaendelea katika kudhibiti mawasiliano ya watuhumiwa kupitia mitandao hiyo katika usafirishaji wa nyara za serikali.

"Tulishawahi kumkamata raia wa Japan ambaye aliwasiliana na mtuhumiwa mwezake kupitia njia ya mtandao wa kijamii Fecbook na wakafanikiwa kununua viumbe hai (kobe) na wakati akisafirisha akakamatwa uwanja wa ndege nchini," alisema.

Pia alisemwa wakati mtuhumiwa huyo anahojiwa, alikiri kwamba alifanya mawasiliano kwa njia ya Facebook na kupata viumbe hao ambao kwa Tanzania ni kosa kumiliki bila ya kuwa na kibali.

Aidha, alisema mizoga ya wanyamapori imepungua tofauti na awali wanyamapori walipokuwa wakiuawa kwa wingi na mwaka 2016 wakati TAWA inaanzishwa, kulikuwa na mizoga 18 kwa mwaka kutokana na tembo kuuawa kutokana na ujangili.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/23 TAWA ilipunguza idadi hiyo na sasa wastani wa mizoga mitatu ya tembo waliuwawa kwa ujangili hupatikana kwa mwaka. Alisema ni mafanikio makubwa ambayo yanatokana na doria na kwa kushirisha jamii katika masuala ya uhifadhi.

Kuhusu tembo yatima na waliotelekezwa, alisema mamlaka huchukua hatua ya kuwapeleka watoto katika kituo cha kuwalea kilichoko Arusha hadi wanapokuwa wakubwa na wanapomudu changamoto za porini, huachiwa.

"Wangeachwa hawa porini wangeshindwa kuishi kwa sababu wanaweza kufa kwa haraka kwa kushambuliwa na wanyama wengine ndiyo maana kikaazishwa kituo cha kuwalea hadi watakapomudu maisha ya kuishi porini," alisema.

Akitoa mada ya uandishi wa habari katika kupambana na uhalifu wa wanyamapori nchini, Mkufunzi kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Abdallah Katunzi, alisema kuna aina kubwa tatu za habari ambazo kila binadamu anahitaji kuzipata zikiwamo zinazuhusu masuala ya msingi kama afya, uchumi na zinazogusa maslahi mapana, hivyo vyombo vya habari vina wajibu wa kuzisambaza.

Katunzi alisema maeneo ya uhifadhi yanagusa maslahi mapana ya jamii na ni maeneo ambayo yanapaswa kuripotiwa na wanahabari kwa sababu uhifadhi na maliasili husaidia katika uchumi wa nchi na wanyama watakapopotea uchumi wa nchi utaporomoka na jamii itaumia.

"Ni muhimu wanahabari kujikita katika katika maeneo haya ambayo yana tija katika jamii yakaweza kutusaidia. Mfano maeneo ya uhifadhi wa mazingira, uhalisia unaonekana kwani mazingira yameharibika na madhara yake yameanza kuonekana, hivyo ni muhimu vyombo vya habari wakazipa ajenda maalum," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema mafunzo hayo kwa wanahabari kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, ni mwendelezo wa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori yanayotolewa na chama hicho chini ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili Tanzania.

Alisema waandishi wa habari ni wadau muhimu katika kuelimisha umma kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira, hivyo ni muhimu wakayafanyika katika kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

## 'Upangaji watumishi uzingatie mwongozo'

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Mahakama imetakiwa kuchukua hatua za haraka kuwapanga watumishi wake kwa mujibu wa miundo ya utumishi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Akikabidhi muundo mpya wa utumishi wa mahakama ofisini kwake, Mwanakwerekwe, Katibu wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Mashaka Kubingwa Simba, alisema lengo la serikali ni kuona mhimili wa mahakama unaleta ufanisi katika usimamizi wa haki na utoaji wa huduma.

Alisema Mahakama inawapanga watumishi wake kwa mujibu wa kada na madaraja yao.

Pia alisema kuna baadhi ya taasisi za serikali hushindwa kuwapandisha madaraja watumishi wao na hivyo kustaafu katika daraja ambalo halistahiki na kumkosesha haki zake.

Aliitaka mahakama kuwapatia mafunzo watumishi wao juu ya kuuelewa muundo huo ili kuutekeleza kwa ufanisi

Naye Mkurugenzi wa Mahakama, Amina Shaibu Mohamed, akipokea muundo huo, alisema katika kuweka utaratibu mzuri wa utumishi wa mahakama, ameahidi kutekeleza mwongozo huo ili kuleta haki kwa wafanyakazi.



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi akiitikia dua ya kumuombea Rais mstaafu Hayati Alhajj Ali Hassan Mwinyi, ikisomwa na Mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hafidh Ameir, alipofika kutoa mkono wa pole, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wanahabari wahamasika tuzo umahiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waanadishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kimesema waandishi wa habari visiwani hapa wamehamasika kuandika na kuwasilisha kazi zao katika tuzo ya umahiri wa waandishi wa habari za wanawake na uongozi zilizoandaliwa na chama hicho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwenye ofisi za TAMWA zilizoko Tunguu, Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar chama hicho Dk Mzuri Issa, alisema ushiriki huo mkubwa unatokana na waandishi kupenda kujituma na kuifanyia kazi jamii.

Alisema kwa upande wa tuzo za mwaka huu juu ya umahiri wa data na uongozi kwa wanawake zilikuwa zinaakisi namna gani ongezeko la wanawake kwenye uongozi katika taasisi mbalimbali wakipata nafasi au kushirikishwa katika vyombo vya uamuzi.

Dk. Mzuri alisema katika tunzo hizo za mwaka 2023 zilizofanyika wiki iliyopita, waandishi wengi walifanya kazi kwa uweledi na kufanya utafiti kabla ya kuandika. Alisema kazi 529 zimewasilishwa katika ushiriki wa tuzo hizo na kwamba idadi imeongezeka na waandishi vijana walionekana kuwa wengi.

Pia alsiema TAMWA imefanya kazi kubwa ya kuwaongezea uwezo waandishi vijana ili kufanya kazi kwa kujiamini na kufuata sheria.

Alisema kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi ya waandishi wa habari vijana 160 walijengewa uwezo wa kufanya kazi kwa ukomavu na kujituma wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

Naye aliyekuwa jaji Mkuu wa tuzo hizo, Dk. Abdallah Mhammed Juma. alisema ushiriki kwa wingi katika tuzo hizo kwa waandishi wa habari wa Zanzibar, kutaibua fursa kwa wanawake kuendelea kujituma na kuwa waledi katika kugombea nafasi za uongozi.

Alisema licha ya kazi nyingi zilizotumwa katika mashindano hayo na kupatikana washindi wachache lakini kazi zote zilikuwa ziko bora na zimefanyiwa utafiti wa kina.



**RAYVANNY**

UKURASA 13

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI MACHI 16, 2024



# WASIOPENDA SHAURI YAO!

NANI kasema kile kilichoonekana Ikulu kwa wasanii maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz na Harmonize, kukaa meza moja na kuzungumza ilikuwa kama mchezo wa kuigiza?

Basi unachoambiwa, yale yaliyoonekana haikuwa kama filamu za kibongo, bali ni kweli wanamuziki hao wameamua kutupa tofauti zao kutoka moyoni.

Jana bosi wa lebo ya Konde Music Worldwide, Harmonize, aliamua kuweka wazi kwamba ameamua kuanza maisha mapya yasiyo na visasi na kwamba ameweka pembeni tofauti zake na Diamond.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Harmonize, amesema akiwa anatimiza miaka 30, anataka kuona anaingia kwenye enzi mpya kama mtu tofauti, asiye na ugomvi au mgogoro na mtu yeyote.

"Usitarajie nifanye mambo yale yale. Nimeamua kuacha kila kitu kibaya. Sikuzaliwa ili kushindana au kupigana na wengine. Upendo wa watu ndio umetufanya kuwa lebo namba moja kwenye majukwaa tofauti ya utiririshaji muziki", alisema.

Harmonize alikwenda mbali kwa kuwaonya watu wanaofikiria kupatana kwao kunaweza kuondoa ladha ya muziki, kwani anachoamini kwake umoja ndio njia pekee ya kuuweka muziki wa Tanzania katika uimara wake.

"Sibishani na watu au kuwaonea wivu. Namruhusu Mungu aongoze njia. Nimeona sehemu ya watu wakisema amani na Diamond itaua mchezo lakini fikra zangu hazikubaliani na hilo kwa sababu sijawahi kuona chuki ikitufikisha katika kiwango ambacho Wanigeria na Waafrika Kusini wamefikia,"ameongeza kusema

Amesema tangu apatane na Diamond amejiona kuwa mtu wa furaha kwa sababu hana kinyongo na anamtanguliza Mungu kwa kila kitu.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aliwakutanisha wasanii hao katika futari aliyoiandaa Ikulu baada ya kila mmoja kuishi kwa chuki kwa miaka mitano tangu Harmonize ajiondoe katika lebo ya WCB ambayo Diamond anaiongoza.

BASI SAWA

## Mwijaku hawezi kuacha uchawa



MSANII wa filamu na maarufu katika mitandao ya kijamii, Mwijaku, amesema ametoka kijijini akiwa masikini, hivyo hawezi kuacha hata senti moja akiwa mjini.

Amesema wanaomsema kutokana na kuwa yeye chawa ni kama wanajisumbua, kwani kila kitu amekipata kutokana na kujipendekeza kwa watu wenye fedha.

"Watu watambue nimetoka katika familia masikini, nilipofika hapa mjini kazi yangu ni kutafuta fedha, waache waniseme kuwa mimi ni chawa lakini nafurahi kuona napata mafanikio mengi kutokana na uchawa wangu,"amesema Mwijaku.

## Mammito haogopi kulaumiwa



MCHEKESHAJI maarufu kutoka Kenya, Eunice Mammito, ameibuka na kuelezea hisia zake baada ya kuachia video inayoonekana kufurahia hukumu ya kifo dhidi ya Jowie.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Mamito amesema ni nadra kwa Wakenya kuungana na kukemea jambo ambalo linaonekana ni muhimu.

Katika video hiyo , alionekana akimshauri Jowie kuona hukumu hiyo kama manufaa kwake binafsi.

Mammito amesema kwa kejeli kuwa kundi hilo linalomlaumu linampa matumaini kuwa siku moja Wakenya wataungana kuzungumza dhidi ya maovu mbalimbali yanayoikumba nchi hiyo.





## DIAMOND, KIBA, HARMONIZE WAJIFUNZE KWA WANIGERIA

WADAU mbalimbali wa muziki wametoa maoni yao baada ya wanamuziki wa Tanzania kuingia katika orodha ya wasanii wanaolipwa pesa ndefu barani Afrika.

Jarida la African Fact Zone, liliwataja wanamuziki Diamond Platnumz, Ali Kiba na Harmonize ni miongoni wanaolipwa pesa nyingi katika kazi zao za utoaji burudani.

Baadhi ya wadau hao wamewataka wasanii hao kuacha uhasama baina yao na badala yake washindane na wenzao wa Nigeria ambao ndio wanaongoza kulipwa pesa nyingi. Burna Boy, Wizkid, Rema kama vinara wa kulipwa mkwanja mrefu kwa kupokea dola milioni moja ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni 2.5.



## Rayvanny anapokumbuka ya WCB

STAA wa muziki wa Bongofleva, Raymond Mwakyusa maarufu Rayvanny, amesema anafurahia kuwa na maisha ya uhuru wa kufanya kazi baada ya kuondoka lebo ya Wasafi.

Rayvanny amesema yeye na bosi wake wa zamani Diamond Platnumz, wana uhusiano mzuri licha ya zoezi la kujiondoa WCB kuwa na hatua ngumu.

"Ilifika wakati niliposema, nadhani ni mzima vya kutosha kuhamia kwangu, kujitegemea, ni vigumu lakini jambo zuri ni kwamba, tuna mawasiliano mazuri. Kwa sababu kwa kawaida wasanii wanapoacha lebo huwa sio nzuri kila wakati," amesema.

## MADEMU HAWA WALITESA SANA DANSINI

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni vigumu sana miaka ya nyuma kuona mtoto wa kike akijihusisha kwenye masuala ya muziki.

Ilichukuliwa kuwa muziki uhuni, na kazi hiyo ni ya wahuni, au watu ambao maisha yao wanayajua wenyewe, hawana mbele wala nyuma na pia watu wasiojiheshimu.

Wazazi wengi hawakutaka watoto wao kujihusisha na masuala ya muziki, na hao ni watoto wa kiume tu, sasa fikiria kwa watoto wa kike inakuaje?

Kwa maana hiyo hakukuwa na wanamuziki wengi wa kike kama ilivyo hivi sasa ambako kumekuwa na wimbi kubwa la wasanii wa kike.

Kwenye miaka ya '80, hadi mwishoni mwaka miaka ya '90, kulitokea wanamuziki waimbaji wachache wa kike ambao mbali na kuwa hawakuwa wengi, lakini waliwawakilisha vema wanawake wenzao kwa kufanya kazi hiyo kwa ustadi mkubwa, uwezo wa hali ya juu kiasi cha kujipatia umaarufu mkubwa nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Na hao ndiyo walioanza kuondoa dhana ya kwamba mtoto wa kike akijiingiza kwenye muziki anakuwa amepotea.

### Tabia Mwanjelwa

Tunaweza kusema kuwa Tabia Mwanjelwa ndiye mama wa waimbaji wote wa kike nchini Tanzania.

Ndiye aliyefungua njia, kwani alianza kuimba kwenye miaka ya '80 akiwa na bendi mbalimbali kama Maquiz Du Zaire na King Kiki Double O.

Anakumbukwa sana kwa nyimbo zake kama 'Maisha ni Safari Ndefu', 'Jeni' alizozirekodi akiwa na Maquiz zinazopendwa hadi leo. Na wakati huo staili za uimbaji kwa wanawake ilikuwa ni kuiga ule wa Miriam Makeba, hivyo nyimbo hizo zina athari hizo.

Aliondoka mwishoni mwa miaka ya '80 na kwenda kuishi nchini Ujerumani.

### Rahma Shally

Ni mmoja wa waimbaji mwenye kipaji cha hali ya juu aliyepata kutokea nchini. Rahma Shally ni mwimbaji pekee wa kike ambaye amefanya kazi na bendi nyingi zaidi kuliko mwingine yeyote nchini. Naye pia aliathiriwa na uimbaji wa Miriam Makeba.

Hii ni kutokana na bendi nyingi kumkubali na kutaka kufanya naye kazi. Amepigia bendi za Mwenge Jazz Band, Vijana Jazz, Sambulumaa na nyingine nyingi.

Aliimba nyimbo kama 'Naomba Tuheshimiane' akiwa na Mwenge Jazz, 'Kaka Saddy' akiwa na Vijana Jazz, pia 'Zamaradi' akiwa na Sambulumaa na nyingine nyingi. Alifariki dunia mwanzoni mwa miaka ya '90.

### Emma Mkello

Alikuwa ni mwimbaji wa kike ambaye hakuathiriwa na uimbaji wa Miriam Makeba. Emma alikuwa na uimbaji wake tofauti kabisa akiwa na sauti nyembamba na nyororo mno, kuliko Rahma Shally au Tabia Mwanjelwa. Huyu alikuwa ni mke wa mwanamuziki maarufu kabisa wakati huo Eddy Sheggy. Hata sauti walifanana yeye na mumewe. Nyimbo kama 'Milima ya Kwetu', 'Kichekesho', 'Hesabu Miaka' na nyingine nyingi akiwa na Super Rainbow, pia "Umbea Sipendelei' aliouimba kwa ustadi wa hali ya juu akiwa na Tanzania Stars 'Watunjatanjata' utunzi wake Ally Choki ulimfanya kuwa bora na maarufu zaidi. Alifariki dunia katikati ya miaka ya '90.

### Nana Njige

Huyu alikuwa ni mwimbaji wa kike ambaye alikuwa na sifa nyingine zaidi ambayo ni urembo.

Alijaaliwa urembo uliwashangaza na kuwapumbaza wanaume wengi wakati huo. Hata jina lake la Nana Njige likageuzwa likawa 'Nana Mzuri.' alipigia bendi mbalimbali kama Super Rainbow na Tancut Almasi na mwishoni kabisa alipigia bendi ya Magereza. Huko anakumbukwa sana alipomba wimbo uliovuma sana uitwao 'Ashura.' Naye alifariki dunia katikati ya miaka ya '90.

### Kida Waziri

Mwishoni mwa miaka ya '80 kuliibuka kipaji cha ajabu kutoka kwa mwanadada Kida Waziri. Aliitingisha nchi kwa vibao kama 'Wifi Zangu Mna Mambo', 'Penzi Haligawanyiki' sehemu ya kwanza na ya pili, 'Wivu' na nyingine nyingi akiwa na bendi ya Vijana Jazz Band.

FILAMU

## Mke bei kali, tamaa hatari

**Na Adam Fungamwango**

TAMAA siku zote ni mbaya. Na kitu chochote ambacho si riziki huwa hakiliki.Kuna baadhi ya binadamu yupo tayari kufanya jambo lolote lile liwe halali au si halali, mradi tu aondoke kwenye sehemu moja kwenda nyingine.

Hata hivyo, chochote binadamu hawezi kufanya bila mipango ya Mwenyezi Mungu. Kama hakupanga, hata ufanye nini ni kazi bure tu.

Haya yamo kwenye filamu ya 'Mke Bei Kali' iliyochezwa Irene Uwoya, Simon Mwapagata, Hemed Suleiman, Patcho Mwamba na wengine wengi. Inaanza kumuonyesha Simon anavyoishi kwa amani na mkewe Irene. Kipato chao kikubwa kinapatikana kwa kilimo na kidogo ufugaji.

Siku mke anatoweka kijijini. Wanakijiji wanakusanyika na kwenda kumtafuta porini kwa kudhani kuwa huenda atakuwa labda ameliwa na wanyama wakali. Mara ya mwisho ilisemekana alionekana anakwenda kuchota maji kisimani.

Wanachofanikiwa kukipata wanakijiji ni nguo zake badala ya Irene awe hai au amekufa. Baada ya miezi kadhaa kupita, zikaja tetesi kuwa Irene ameonekana mjini.

Taarifa zinaanza kuwa za kuanza kuaminika. Simon anaamua kwenda mjini kumsaka Irene. Wanapofika huko wanaishi maisha ya kubangaiza.

Siku moja akiwa anaangalia televisheni, Simon alimuona Irene akiwa na mwanamuziki maarufu nchini Hemed. Na hapo ikatangazwa kuwa mwanamke huyo ni mke wa Hemed.

Hakuamini macho yake. Mkewe leo kageuka kuwa mke wa mwanamuziki mkubwa nchini. Anaulizia anakoishi Hemed. Anafika nyumbani kwake na nia kujua nini kilitokea hadi ikawa hivyo.

Anatimuliwa kama mbwa. Irene licha ya kudai kuwa si mumewe, lakini maisha yake hajawahi kuonana na mtu kama huyo.

Simon anaondoka na kuendelea na maisha yake. Irene akazidisha makuu, akaanza kuwa na mahusiano na bosi wa Hemed ambaye ni Patcho Mwamba.

Hakutosheka, akawa kiruka njia haswa. Wakati huo Hemed alikuwa kwenye ziara za muziki. Aliporejea alipata taarifa ya kuwa promota wake ana uhusiano na mkewe. Akamtimua mke na kujiondoa kuwa chini ya Patcho na kuanza kujitegemea mwenyewe.

Irene kwa kuchanganyikiwa alianza kujiingiza kwenye matumizi ya madawa ya kulevya. Mume wa kweli Simon alipopata taarifa akamtafuta mkewe na kumpeleka kwenye kituo cha afya ili kupata tiba. Irene alipopona, alichukuliwa na mumewe Simon na wote wakarejea kijijini kuanza tena maisha mapya.



BT BURUDANI TELE



# Edebiri ashindwa kujielewa

MWIGIZAJI wa Marekani mwenye asili ya Nigeria, Ayo Edebiri, amesema umaarufu anaopata kutokana na kazi yake imemfaya kujiona kama kichaa.

Akizungumza na jarida la Vogue, Edebiri, amesema filamu yake 'The Bear' imembadilisha maisha yake na kuwa maarufu zaidi kiasi ambacho anashangazwa nacho.

Amesema aliposafiri katikati ya msimu wa joto wa 2023 kwenda jijini Berlin na marafiki zake, yeye alikuwa akizuiliwa mara nyingi na mashabiki wa filamu.



## Hii ndio furaha ya mama

NYOTA wa filamu kutoka Nollywood, Iyabo Ojo amemfanyia 'sapraizi' binti yake baada ya kualika bendi ya muziki kwa ajili ya kuburudisha siku yake ya kuzaliwa.

Katika video zilizosambaa mitandaoni, inamuonyesha mwigizaji huyo na binti yake wakiingia katika ukumbi huku bendi ya muziki ikitoa burudani iliyomfanya mwanawe huyo kuwa na furaha zaidi.

Katika ukurasa wa Instagram wa Ojo, alichapisha picha za binti yake huku akielezea jinsi alivyomfanya mtoto wake kushangazwa na kile alichoona katika ukumbi huo uliojumuika watu maarufu nchini Nigeria.

## Kivazi cha Ice Spice hatari!

RAPA mwenye utata kutoka Marekani, Ice Spice amekuwa gumzo baada ya vazi lake alilovaa katika sherehe ya utoaji tuzo za Oscar kuwashangaza watu.

Ice Spice aliingia katika ukumbi akiwa na gauni jeusi linaloonyesha umbo lake lote na kusababisha watu waliokuwa ukumbini kuonyesha sura za mshangao.

Rapa huyo ambaye mara nyingi anakuwa na vituko ili kuonyesha uwepo wake, hakuonyesha hali ya wasiwasi wakati aliposimama katika zuria jekundu kwa ajili ya kupiga picha, badala yake alitembea kwa madaha kuelekea sehemu ambayo alitakiwa kukaa.





## Funsho ukipewa nafasi utaiacha?

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Funsho Adeolu, amesema kamwe msanii wa filamu hawezi kuwa mwanasiasa mahiri.

Akizungumza katika kipindi cha mchekeshaji Babyface, Adeolu alisisitiza kuwa uigizaji na siasa haviendani na wanaofanya hivyo watakuwa wanapotoka.

"Watu wakiniita mimi mtu mashuhuri, nasema hapana mimi ni muigizaji, kwangu mimi ni muigizaji na hao wengine wote wanakuwa wanasiasa sio waigizaji, mwigizaji hawezi kuwa mwanasiasa," aamesema.

## Ushauri wa Rita uzingatiwe

MKALI wa filamu za Nollywood, Rita Edochie, amewashauri wazazi na walezi watarajiwa nchini Nigeria kujitunza kila wakati kuhusu malezi kwa ajili ya watoto wao.

Mwigizaji huyo maarufu alitumia ukurasa wake wa Instagram, kueleza kwamba sio jambo zuri kwa watoto kushindwa kumudu maisha baada ya kifo cha wazazi wao.

Ameeleza hakuna mtu mwingine anayeweza kutunza watoto au kuwa mchungaji bora kwao kuliko wazazi wao wa kibaiolojia, hasa wakiwa bado wadogo.





## Wapewa mbinu kupambana na dawa za kulevya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imekutana na watoa huduma za usafirishaji wa abiria katika mkoa wa Arusha na kuwapa mbinu za kuwabaini abiria wanaoficha dawa za kulevya ndani ya mizigo yao.

Mpango huo unalenga kuwawezesha makondakta na madereva kutambua mizigo yenye dawa za kulevya zinazosafirishwa kupitia vyombo vyao vya moto.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa DCEA Kanda ya Kaskazini, Sara Ndaba, alitangaza kuwapo kwa operesheni hiyo, alipoalikwa kwenye kikao cha wadau wa usafirshaji kilichoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA).

Alisema kikao hicho na mwendelezo wa vingine, vinalenga kutoa elimu juu ya kanuni mpya za usafirishaji.

"Mkakati wa kwanza uliopo mbele yetu ni kupunguza uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya ,kupitia elimu tunayoitoa leo, kwa sababu vyombo hivi vya usafiri, vinatumika mno, kusafirisha dawa za kulevya ikiwemo mirungi na bangi,"alisema.

Alisema ili kudhibiti hilo, wamekna kuna umuhimu wa kutoa elimu hiyo kwa wadau wa usafiri Mkoa wa Arusha, ili wapatiwe elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya na jinsi ya kubaini miziho hiyo kwenye vyombo vyao.

Alisema kwa kushirikiana pamoja na wadau hao, itasaidia kukomesha usafirishaji huo na kunusuru vijana ambao baadhi yao wanaangamia katika lindi hilo.

Ofisa Elimu Jamii wa DCEA, Shaban Miraji, alisema wadau wa usafirishaji ni kundi muhimu kupata elimu hiyo, kwani wanahusika kwa kiasi kikubwa kusafirisha mizigo na baadhi yao kusambaza dawa za kulevya.

"Vyombo hivi vinatumika sana kusafirisha dawa za kulevya, ili dawa za kulevya ziweze kuenea nchini, lazima vyombo vya usafiri vitumike kusambaza kwa mfano mihadarati aina ya mirungi inapitishwa katika mpaka wa Namanga kupitia mabasi ama pikipiki, hivyo hii ni hatari,"alisema.

"Kwa hiyo baada ya kubaini hili tumeamua kuja kutoa elimu hii, ili wadau wa usafiri watambue namna ambavyo vyombo vyao vinatumika kusafirisha dawa za kulevya, iwe kwa kujua ama kwa kutojua.

"Vizuri mkatambua sheria za mamlaka hii, ni kali iwapo utabainika chombo chako kinahusika katika biashara hiyo haramu, adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 na chombo chake kinataifishwa na kuwa mali ya serikali,"alisema.

Mwenyekiti wa Waendesha Pikipiki (Bodaboda), Wilaya ya Arusha, Okelo Costantine, alisema sekta ya usafirishaji hasa bodaboda ina changamoto nyingi, ikiwemo kusafirisha dawa za kulevya bila kujua.

Alisema semina hiyo itawawezesha kuelimisha wenzao jinsi ya kuepuka usafirishaji wa dawa hizo na kuwachukulia hatua stahiki wahusika, kwa sababu baadhi ya viongozi wanafahamu wapo baadhi wa waendesha pikipiki, wanahusika kusafirisha dawa za kulevya.

# Mtaalamu aibua madhara kilimo kwa afya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MTAALAM wa kilimo ikolojia, Fredrick Ochieng, amesema kilimo kinachotumika hivi sasa katika nchi za Afrika Mashariki kwa ajili ya kuzalisha mazao ya chakula, si rafiki kwa afya za watu.

Ochieng ambaye ni raia wa Kenya, amesema kilimo hicho huchangia magonjwa ya binadamu, kudhoofisha ubora wa ardhi na kuwa tegemezi.

Ochieng, Mratibu wa Programu wa Taasisi ya Biovision Africa Trust (Tanzania), alikuwa akizungumzia umuhimu wa kilimo ikolojia (kilimo hai), alipokutana na wadau wa kilimo hicho.

"Kilimo ikolojia kimeboresha maisha ya wakulima wengi kwa kupata faida ya mazao yao na lishe bora.

Ni vyema sasa tukahamasisha wakulima kujikita kwenye uzalishaji wa aina hiyo, badala ya hiki kilimo cha sasa,"alisisitiza.

Naye Meneja Mradi wa Mkulima Mbunifu, Erica Rugabandana, alisema huduma za mkulima mbunifu zimepanuka na kuwafikia zaidi ya wakulima 100,000 kupitia majarida na kupitia mawasiliano ya simu.

"Tumekuwa tukipokea ujumbe wa simu na kupokea ujumbe kutoka kwa wakulima wengi, ambao wanasoma majarida ambayo yanatolewa bure," alisema.

Mmoja wa wadau, Penina Nnko, kutoka Halmashauri ya Meru mkoani Arusha, alisema kilimo ikolojia kimekuwa na manufaa makubwa kwao, kwa sababu wamekuwa wakinufaika na elimu.

Akijibu hoja za wadau hao, Ofisa Kilimo Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Rose Massawe, aliwashauri wakulima nchini kuanza kutumia mbegu za asili katika kilimo ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ambayo kinapunguza uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Aliwataka kutodharau maelekezo ya wataalam wa kilimo na kushirikiana na watafiti wa kilimo, ili kuwasaidia kutumia mbegu bora za asili ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Massawe alisema ni muhimu wakulima kupata taarifa sahihi za kilimo Ikolojia ikiwepo matumizi ya mbegu bora za asili ambazo ni rafiki kwa mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), Janet Maro, alisema warsha hiyo ni muhimu kwa wakulima na wadau wa Kilimo Ikolojia nchini.



Fundi mchundo wa kiwanda cha ufuaji wa chuma cha Kilimanjaro Machine Tools Manufactures Ltd, Anna Mosha (kushoto), akitoa maelezo kuhusu utengenezaji wa vipuli na mitambo kwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara Kilimo na Mifugo, walipotembelea kiwanda hicho, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Adha ya usafiri yapatiwa ufumbuzi

**Novatus Makunga,** ARUSHA

ADHA ya usafiri wa barabara kwa wananchi wanaotumia mabasi na watalii wanaotumia magari maalum yanayotoa huduma kupitia eneo korofi la Engaruka na Engarasero katika wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, imepatiwa ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Arusha, Reginald Massawe, eneo hilo lenye urefu wa kilometa 39, litajengwa kwa kiwango cha lami wakati wowote kuanzia sasa.

Kipande hicho, ndicho kinachokatisha katika Mlima Oldonyolengai, ambao una volkano hai, Bonde la Ufa na Ziwa Natron, lenye maji ya magadi. "Ni kweli tumeanza mkakati wa kukamilisha ujenzi wa kilomita 217 kwa kiwango cha lami katika barabara inayopita katika maeneo magumu ya mabonde na miinuko mikali, hasa pembezoni mwa Mlima Oldonyolengai,

"Ziwa Natron na Bonde la Ufa, inayolenga kuunganisha makao makuu ya mkoa yaani jiji la Arusha na makao makuu ya wilaya ya Ngorongoro, mji wa Loliondo," alisema. Meneja huyo alisema mkakati huo ni pamoja na kuugawa ujenzi wa barabara hiyo katika awamu nne, ili kukamilisha malengo ya serikali ya kuunganisha makao makuu ya mikoa na makao makuu ya Wilaya, kwa lengo la kuimarisha uchumi na shunguli za kijamii.

Katika Mkoa wa Arusha ni wilaya moja tu ya Ngorongoro ambayo makao makuu yake mji wa Loliondo, haifikiki barabara ya lami.

Alisema ujenzi wa awamu ya kwanza kati ya Wasso na Sale yenye urefu wa kilometa 49 kwa kiwango cha lami, ulikamilika mwaka 2022 kwa gharama ya Sh. bilioni 87.

Massawe pia alisema maandalizi ya kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya Mto wa Mbu hadi Selela, yenye urefu wa kilometa 23, umeanza kwa zabuni kutangazwa na kufunguliwa Machi 14 mwaka huu.

Alisema awamu ya tatu, kati ya Wasso na Loliondo, yenye urefu wa kilometa 10, nayo zabuni imetangazwa na iko katika hatua za mwisho.

Kwa upande wa awamu ya nne yenye kipande kigumu zaidi kati ya Engaruka na Engarasero, alisema tayari

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Enzi za mchezo wa redio, visa vya mzee Jongo na Jangala redioni

Na Adam Fungamwango

SIKU hizi utaona familia imekaa varandani imetulia, inafuatilia tamthilia au filamu kwenye televisheni. Zamani haikuwa hivyo. Hakukuwa na televisheni wakati huo Tanzania Bara. Televisheni Bongo zilianza kuingia mwanzoni mwa miaka ya 1990. Tena kwa watu wachache tu, kwenye nyumba ishirini unaweza kuikuta kwenye nyumba moja mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Miaka ya mwanzoni mwa 1990 hata zilipoingia hakukuwa na vituo vya televisheni.

Wengi TV walizitumia kwa kuangalia mikanda ya video. Ndiyo wakati ilipoingia mikanda mingi ya picha za kizungu, kihindi, pamoja na miziki kutoka Congo DR, hasa ya kina Aurlus Mabele, Kanda Bongomani, Pepe Kalle, Soukous Stars, na zingine nyingi.

Wakati nchini ikiwa bila TV, kitu pekee ambacho kilichokuwa kikiwahabarisha Wabongo ni redio. Tena nazo huwezi kukuta kila mtu anayo. Vijijini inawezekana anawa nayo Mwenyekiti wa Kijiji tu. Na ilikuwa ni vipindi maalum na wakati husika wa kwenda kusikiliza.

Walimu, na watu waliokuwa wakifanya kazi serikalini, au bomani, ndiyo walioonekana kumudu kuwa nazo.

Siyo mikoani tu, hata Dar es Salaam. Unaweza kutembelea nyumba 10 ukakuta moja tu ndiyo yenye redio.

Zilipoingia televisheni, nchi ilipata mastaa wa tamthilia na filamu kama kina Steven Kanumba, Ray Kigosi, Wema Sepetu, Irene Uwoya na wengine wengi.



Mwigizaji maarufu wa siku nyingi nchini, Bakari Mbelemba, maarufu kama Mzee Jangala

Hawa walikuwa wanaonekana kwa macho, baada ya kuingia kwa televisheni. kabla ya hapo kulikuwa na mastaa wa michezo ya kuigiza.

Hawa hawakuwa wanaonekana kwa macho. Hawa walikuwa wanasikika tu kwenye redio. Lakini michezo yao ilikuwa maarufu sana wakati huo na wao kuwa maarufu. Kwa bahati mbaya hata wakionekana kwenye macho ya watu hawajulikani. Labda mpaka uambiwe huyu ndiyo fulani. Hawa ndiyo mastaa wa zamani.

Moja kati ya waigizaji waliokuwa maarufu wakati huo ni Ibrahim Raha ambaye alijulikana kwenye michezo ya kuigiza kama Mzee Jongo. Mwingine ni Bakari Mbelemba, ambaye yeye alijulikana kama Mzee Jangala.

Ni waigizaji waliojichukuliwa umaarufu mkubwa wakati huo kutokana na aina yao ya uigizaji.

Mzee Jongo ambaye ni marehemu, alikuwa ni mzee mwenye vituko, mtata, ambaye pia alikuwa na tabia ya kumweleza ukweli mtu hapo hapo, bila kuzungisha maneno au kusubiri wakati fulani.

Lafudhi yake ya Kizaramo ilikuwa burudani tosha, pamoja na kushindwa kutamka baadhi ya maneno ya kiswahili kwa ufasaha.

Kuna mchezo mmoja wa jamaa ambaye alimtelekeza mkewe kwenda kuishi kwa kimada, lakini baada ya pesa kumalizika alirudi kumuomba radhi mkewe. Mzee Jongo ni mmoja wa wazee walioitwa ili kumaliza tatizo hilo. Jamaa akawa anamwambia mkewe "mke wangu nipokee."

Mzee Jongo akamwambia "We muombe vizuri mkeo ili akusamehe, unamwambia akupokee, kwani umekuja na treni?" Hivi ni moja kati ya vituko vya mzee huyo.

Mchezo mwingine ni wa jamaa aliyekuwa mwizi. Alikwenda kuiba bandarini wakamkamata, wakampiga na kulazwa Muhimbili. Majirani walipoambiwa waliogopa kwenda kumpa habari mkewe.

Mzee Jongo kama kawaida yake akajitolea akaenda kumwambia "Mumeo kenda homola bandarini. Basi wamemkamata. Wamembomoa kweli kweli. Ukimuona mumeo hivi sasa utamsahau. Mumeo kana songo. Migulu bogojo. Mizino fumu."

Hapa alikuwa alimpa habari mke wa jama huyo mwizi kwa kiswahili kilichochanganyika na kizaramo.

Alikuwa anamwambia mumewe ameenda kuiba bandarini, wamemkamata na kumpiga. Mumewe sasa ana chongo. Miguu imevunjwa na baadhi ya meno yametoka.

Ilifika wakati mchezo wa kuigiza wowote wa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) bila mzee Jongo kwa mashabiki ilionekana kama haujakamilika.

Mwingine ni mzee Jangala. Huyu bado yupo. Tabia zake hazitofautiani sana na mzee Jongo. Ni mtata. Yeye lafudhi yake ni ya watu ya Rufiji mkoani Pwani na kidogo kama Ifakara mkoani Morogoro.

Ni mzee mtata, mbishi mwenye msimamo mkali. Alikuwa na uwezo wa kusimamia anachokiamini hata kama atakuwa peke yake watu wote waliobaki wako upande mwingine.

Moja ya mchezo wake au igizo lake kwenye redio liliitwa 'Niachieni Mwenyewe.' Alikuwa na kijana wake Mshamu ambaye alimdekeza kupita kiasi. Lakini baadaye matokeo yake aliyaona.

Kingine ni kwamba mzee Jangala hata kama atasimamia jambo ambalo liko kinyume na jamii na watu wote hawakubaliani nalo, bado ana uwezo mkubwa wa kujenga hoja nzito kulihalalisha, kiasi kwamba hata baadhi ya wanaosikiliza wanaweza kuamini kuwa yuko sahihi. Hii ndiyo maana halisi ya mwigizaji au msanii.

Wasanii hawa wawili walisababisha watoto, vijana na akinamama siku ya mchezo kufanya kazi zao mapema na kukaa kusubiri muda wa mchezo wa kuigiza.

Walisaidiana na baadhi ya wasanii kama Janja, Zena Dillip maarufu kama Siwema Binti Mtayaona, ambaye uigizaji wake haitofautiani sana na Bi.Hindu. Wengine ni Hamisi Tajiri, Ally Keto, Mzee Igunanilo na wengineo.

**Tuma meseji 0716350534**

HABARI KIMATAIFA

# Viongozi wa upinzani Senegal waachiwa

**DAKAR,** SENEGAL

RAIS wa Senegal Macky Sall, ametoa amri ya kuachiwa kwa msamaha kwa viongozi wa upinzani ambao walikuwa wamefungwa gerezani kwa makosa mbalimbali.

Viongozi waliopata msamaha huo ni Ousmane Sonko na mgombea urais anayemuunga mkono katika uchaguzi ulioahirishwa Bassirou Diomaye Faye.

Viongozi hao wa upinzani waliachiwa jana na wawili hao walipokewa na mamia ya wafuasi wao waliokuwa na furaha katika mji mkuu wa Dakar.

Kuachiwa kwao kunatokana na msamaha uliotangazwa na Rais Macky Sall juzi.

Uchaguzi huo unatazamiwa kufanyika Machi 24, mwaka huu baada ya kuahirishwa kwa kile kilichoelezwa kuwapa nafasi wagombea waliokosa fursa hiyo kushiriki.

"Ni siku nzuri zaidi maishani mwangu," mfuasi mmoja aliambia BBC.

Faye, mwenye umri wa miaka 44, ambaye ni mmoja wa wagombea 19 wanaoshiriki uchaguzi huo, anawania kupitia chama cha muungano cha Rais Sall.

# Watu 20 wauawa wakisubiri msaada wa chakula Gaza

**GAZA,** PALESTINA

WATU 20 wameuawa na wengine 155 wamejeruhiwa baada ya majeshi ya Israel kushambulia Wapalestina waliokuwa wakisubiri msaada wa chakula.

Katika tukio hilo lililotokea jana, vifaru na ndege za helkopta zilitumika kufanya shambulizi hilo katika mji wa Gaza.

Wizara ya afya inayoongozwa na Hamas, iliwashutumu wanajeshi wa Israel kwa kufyatua risasi wakati watu waliokusanyika kaskazini mwa Gaza wakisubiri msaada wa chakula.

Mohammed Ghurab, mkurugenzi wa huduma za dharura katika hospitali moja kaskazini mwa Gaza, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba vikosi vya uvamizi vilifyatua risasi kwa watu ambao walikuwa wakisubiri msaada huo.

Mwandishi wa habari wa AFP aliyekuwa kwenye eneo la tukio alishuhudia miili kadhaa ya watu pamoja na majeruhi wakiwa wamelala ardhini.

Hata hivyo, jeshi la Israel limekanusha kuwafyatulia risasi raia na kueleza kuwa taarifa hizo ni za uongo na inatathmini tukio hilo kwa umakini.

Wakati hayo yakijiri, Umoja wa Mataifa umeonya juu ya tishio la baa la njaa katika Ukanda wa Gaza.

Juhudi za mbalimbali za kuwasilisha chakula na misaada mingine zimeongezeka kwa kutumia njia tofauti za angani na baharini kwa kupitia katika nchi za Jordan, Israel na Misri.

Mashuhuda walisema meli ya misaada ya Uhispania ya Open Arms, iliyokuwa na shehena ya tani 200 za chakula kilichotolewa na shirika lisilo la kiserikali la Marekani World Central Kitchen (WCK), imewasili katika pwani ya Gaza mchana wa jana.

Hata hivyo, imeripotiwa kuwa mapigano makali yanaendelea baada ya wapatanishi kushindwa kufikia makubaliano ya usitishwaji mapigano katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sisi, alisema kuwa nchi yake inaendelea na juhudi za kujaribu kufikiwa kwa mpango wa kusitisha mapigano ambao utaruhusu kuingizwa kwa misaada zaidi na kuwawezesha watu waliohamishwa kusini mwa Gaza kurejea eneo la Kaskazini. Kwa upande wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu amepuuza uwezekano wa kupatikana kwa mapatano baada ya Hamas kutoa masharti kwa wapatanishi.

Ofisi ya Netanyahu ilisema kuwa Hamas bado inashikilia madai ambayo hayatekelezeki.

Aidha, kiongozi wa Bunge la Seneti nchini Marekani Chuck Schumer, alitoa wito wa kufanyika kwa uchaguzi mpya nchini Israel, huku akimshutumu Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu kwa kutanguliza maslahi yake ya kisiasa badala ya nchi hiyo.

Schumer, ambaye ni mwanachama wa chama cha Democratic na Ofisa wa ngazi ya juu wa Kiyahudi nchini Marekani, alisema Netanyahu amepoteza mwelekeo.

Alionya kwamba idadi kubwa ya majeruhi Ukanda wa Gaza inatishia kuleta mvutano baina ya washirika na kuifanya Israel kutengwa kimataifa.

Ukosoaji huo unaelezwa ni wa kwanza mkubwa kutoka kwa kiongozi wa kisiasa wa Marekani dhidi ya serikali ya Netanyahu.

**DW**



Wafuasi wa kiongozi wa upinzani nchini Senegal, Ousmane Sonko wakishangilia kuachiwa kwake katika jiji la Dakar jana.
**PICHA: AFP**

# Raia Russia wapiga kura kumchagua rais

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIA wa Russia wanapiga kura katika uchaguzi wa rais utakaofanyika kwa muda wa siku tatu.

Rais wa nchi hiyo, Vladimir Putin anatarajia kupata ushindi na kuongoza kwa muhula mwingine wa miaka sita.

Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa jana saa mbili asubuhi katika maeneo yote ya nchi hiyo na vitafungwa Jumapili saa mbili jioni.

Katika ujumbe wake kabla ya kufanyika Rais Putin, aliwataka raia kumuunga mkono licha ya taifa hilo kupitia katika kipindi kigumu.

Matumaini ya kiongozi huyo yameongezeka wakati wanajeshi wakipata ushindi wao wa kwanza kwenye uwanja wa vita nchini Ukraine baada ya kupita mwaka mmoja.

Katika uchaguzi huo rais Putin hana upinzani mkali kutokana n a viongozi wengi wa vyama vya upinzani kuuawa au kufungwa jela. Uchunguzi wa maoni uliendeshwa na kituo cha televisheni cha serikali ulionyesha kiongozi huyo atapata zaidi ya asilimia 80 ya kura.

Ushindi huo utamruhusu kukaa madarakani hadi 2030, ukiwa muda mrefu zaidi kuliko kiongozi yeyote wa Russia tangu Catherine the Great katika karne ya 18. Raia wanapiga kura kwenye vituo karibu 100,000 ndani ya taifa hilo na yale yaliyochukuliwa na Russia nchini Ukraine katika vita vinavyoendelea.

Mkuu wa eneo la Crimea, Sergei Aksyonov, alisema uchaguzi huo utaonyesha mustakabali mwema wa Russia katika kipindi kinachokuja.

"Nimepiga kura hivi punde kwa mustakabali wa Urusi. Hali ni nzuri. Kila kitu kinakwenda kulingana na mpango. Tunapiga kura kwa mustakabali wa Russia, usalama, maendeleo ya kiuchumi, maisha na afya ya watoto na wajukuu zetu." Alisema.

Wakati huo huo, watu wawili wamejeruhiwa katika mashambulizi yaliyofanyika jana kwenye mpaka wa Russia na Ukraine karibu na mji wa Belgorod.

Kupitia mtandao wa Telegram Gavana wa eneo hilo, Vyacheslav Gladko, alithibitisha tukio hilo huku Wizara ya Ulinzi ya Russia ikisema kuwa makombora saba ya yalivurumishwa Belgorod kutoka Ukraine.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABEID IDDI SIMAI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NS. 5171/186** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MPENDAE SEKONDARI SKULI** mwaka **2017.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA : PHQ/DAR/KIG/36488/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**VANESSA WILBERT MHINA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye namba TAE 465681 iliyotolewa makao makuu **DAR ES SALAAM PCO** mwaka **2022.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/35958/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya BAGAMOYO**
**Kituo cha KEREGE**
**Mkoa PWANI**
**Shauri la madai Na 55/2023**
**Jina la mdai MIKIDADI YUSUPH RWESHABULA**
**Jina la mdaiwa OTHMAN ALLY SHOMARY**
**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

**KWA OTHMAN ALLY SHOMARY**

Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe....nwezi....mwaka....kueleza kwanini HUkumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 4 Mwezi 3 Mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KEREGE - BAGAMOYO

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**MAOMBI MADOGO NA. 197 YA 2023**
**PETER ZAKARIA WAMBURA......... MLETA MAOMBI**
**(Msimamizi wa mirathi ya marehemu Juma Masai Wambura)**
**DHIDI YA**
**CHARLES NDESI............MJIBU MAOMBI**
**CHARLES NDESI**

**POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba mleta maombi **PETER ZAKARIA WAMBURA** ameleta Maombi madogo ya kukazia hukumu **Na. 197/2023,** dhidi yako.

Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa kuleta majibu yako na uwepo barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, tarehe **20/03/2024,** siku ambayo shauri limepangwa kutajwa.

Endapo hutatekeleza hayo, shauri litaendelea upande mmoja dhidi yako na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwea saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe **27/02/2024.**

MAHELELE M.S
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu HUSNA MELIKIONI NCHIMBI** anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki aina ya Sanlg zenye usajili namba **MC585 BPJ** na **MC477BQH.** kwa yeyote atakayeziona anaombwa atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu nae.

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/TAN/HAN/2074/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**OFISI YA HAKIMU MKAZI,**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA TEMEKE**
**S.L.P 46266,**
**DAR ES SALAAM**

**YAH : KUITWA SHAURINI/GAZETINI**
**MADAI NO. 45/2022**
**MDAI: TATA AFRICA HOLDINGS(TANZANIA ) LTD**
**MDAIWA: GEMIN ENGINEERING & CONSTRUCTION LTD**

Madai hayo yamefunguliwa katika Mahakama hii Ndugu Gemin Engineering & construction LTD Unaamriwa na mahakama hii kuhudhuria mnamo tarehe 18/3/2024 na usipohudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA TEMEKE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 4359/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**ANNA ALBERT MWAKAMOJA**
**AND**
**In the matter of Application for letters of administration by GROLIA RASHIDI MWAKALINGA...............PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 2nd day of April 2024

Dated at Kyela this 4th day of March, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

---

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-4

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Kamal alijiingiza kwenye mitaa ya vijijini, lakini hakuwa mnywaji wala mvuta sigara, hivyo dakika 10 zilimtosha huko na akarejea tena eneo la barabara ya Morogoro kusubiri matengenezo ya basi.

Katika angalia yake, akamuona msichana aliyekaa naye siti moja amekaa peke yake kwenye nyasi akili yake yote ikionekana kwenye simu yake.

Akaamua kusogea kwa hatua za taratibu kuelekea alipo. Mariamu hakutambua kama kuna mtu anamfuata.

Alipofika karibu yake, akiwa nyuma ya mgongo wa anayemfuata alisimama. Alibakisha kama hatua tatu za mtu mzima kufikia.

"Vipi, mrembo, mbona umekaa huku peke yako?"

Sauti hiyo nzito kidogo na yenye utulivu ikionekana haina chembe ya wasiwasi, ilimshtua Mariamu aliyekuwa makini kuangalia vikatuni kwenye simu yake ya mkononi.

Macho yake yalikutana na mtu yule yule aliyemkwaza ndani ya basi. Akakunja sura kwa namna ya kauonyeha hakupendezwa kwa mgeni yule kufika pale.

Akamuangalia kuanzia chini na kumpandisha hadi juu. Halafu akafyonya.

Kamal alitabasamu. Lilikuwa ni tabasamu halisi ambalo lijidhirisha wazi kwa Mariamu.

Halikuonekana la kupooza hasira ya kufyonywa. Wala halikuonekana kuwa la kujibaraguza. Lilionekana ni la mtu asiyejali chochote. Ilimshangaza na kuzidi kumkera Mariamu.

"Huyu ni mwanaume gani asiyekuwa na hisia ya kitu chochote?" Akajiuliza.

Alidhani akifanya vile anaweza kumkera Kamal akaondoka, au kuanza kuzozana ili kuendeleza kile kilichotokea ndani ya basi. Haikuwa hivyo.

"Mwanamke mzuri na mrembo kama wewe hupaswi kufanya hivyo." Lilikuwa jibu la kile alichofanyiwa. Akajibu huku akipiga tena hatua moja mbele.

"Dada, nikwambie kitu." Kamal aliongea kwa sababu ya chini. "Siyo kama kuna kitu nataka, au naomba kutoka kwako, au nataka suluhu au kukuomba msamaha. Ila tu nataka nikuhakikishie kuwa nilichokifanya ndani ya basi hakikuwa kitu halisi!"

Mariamu aliinua macho yake meupe ya duara, akamtazama kwa mshangao, lakini yalikutana na macho ya Kamal, ya mwanamama huyo yakashindwa kuhimili vishindo, akayarudisha chini.

Moyoni mwake alikuwa anajiuliza alikuwa na maana gani kusema vile. Awali hakutana kabisa kumsemesha. Lakini maneno ya Kamal yalikuwa kama yana fumbo fulani ambalo lilimkereketa na kutaka kujua.




**"Ukweli unabaki pale pale kuwa mimi nilipanda hili basi, nikachagua ile siti, nikakaa dirishani, kwa sababu lilikuwa lina abiria wachache nikaamua kuteremka kwanza ili kupunga upepo na kunyoosha kidogo miguu kwa sababu nilijua nikirudi nitakaa hapo kwa muda mrefu, kumbe wewe ukapanda na kwenda kukaa kwenye ile siti, sasa abiria walikuwa wanasubiri udhaifu wa mwanaume, nashukuru hakuona, ndiyo maana walishangaa sana."**

"Una maana gani ukisema siyo kitu halisi?" Akauliza Mariamu huku akiwa hamtazami Kamal, lakini akiwa amefura kwa hasira.

Hicho ndicho alichokuwa anakitaka Kamal. Ni kupewa nafasi ya kuzungumza na kusikilizwa.

"Nilipopanda basi abiria wote walioniona nimeshuka kabla basi halijaondoka pale Msamvu, walianza kunitazama sana, wengine walitabasamu, wengine wakacheka.

Mimi nikashangaa, hawa mbona wananiangalia sana wengine wakacheka? Kuna nini? Kufika kwenye siti yangu nakuona wewe. Kwa jinsi nilivyokutazama tu sura na ulivyo, nikajua sababu.

Unajua wewe ni msichana mrembo sana, Mungu kusema kweli amekujaalia, sasa nikagundua kuwa wale waliona nikifika pale na kukuta umekaa siti yangu nitanywea, nitakaa kwenye siti ile ile, lakini pembeni, siyo kule dirishani. Ndiyo kitu ambacho walikuwa wanasubiria." Kamal aliongea kwa sauti ndogo, lakini ya wazi na ya msisitizo, iliyoonekana haikuwa na chembe ya udanganyifu.

"Nikaona ahaa hawa wanajua kuwa nikifika kwa msichana kama wewe nitakuwa mnyonge na dhaifu, sasa ngoja niwaonyeshe, ndiyo nikaanza ile purukushani ulioyoiona, ukweli ni kwamba ilikuwa ya kuigiza ili kuwashangaza waliokuwa wanadhani kitakuwa kile ambacho kingekuwa."

Mariamu alishusha pumzi, lakini akabaki kimya bila kusema neno lolote.

"Ukweli unabaki pale pale kuwa mimi nilipanda hili basi, nikachagua ile siti, nikakaa dirishani, kwa sababu lilikuwa lina abiria wachache nikaamua kuteremka kwanza ili kupunga upepo na kunyoosha kidogo miguu kwa sababu nilijua nikirudi nitakaa hapo kwa muda mrefu, kumbe wewe ukapanda na kwenda kukaa kwenye ile siti, sasa abiria walikuwa wanasubiri udhaifu wa mwanaume, nashukuru hakuona, ndiyo maana walishangaa sana."

"Sasa wewe mwenyewe ndiyo unaona umefanya vizuri?"

"Hapo kuna pande mbili. Kwangu mimi binafsi nimefanya vizuri sana. Nimeonyesha kuwa bado duniani kuna wanaume wenye misimamo na si dhaifu kama wanavyodhani, lakini bila kupepesa macho ni kwamba nimekukwaza."

"Siyo umenikwaza umenidhalilisha pia."

"Ni kweli, kwa hilo naomba msamaha, lakini sijutii nilichokifanya, kwa sababu nilifanya kwa makusudi, lakini nia yangu haikuwa ile, narudia tena hakikuwa kitu halisi, niliigiza, ningeweza kukuacha kukaa pale dirishani, sina ugonjwa wa kutapika wala nini. Macho ya watu walifanya nifanye vile."

"Na unaendelea kujisifia."

"Ndiyo, kwa sababu nimejiwekea heshima, lakini na wewe naweza kubadilisha hicho unachokisema ukapata heshima pia kwa abiria wote mle ndani."

"Utafanya nini?" Akazidi kuuliza Mariamu ambaye kila muda aliokuwa akiongea na Kamal ni kama hasira zilizidi kupungua.

"Utaona mwenyewe basi likishatengenezwa tukipanda mle ndani."

Mara akapita muuza samaki wa kukaanga. Alikuwa akiwauzia baadhi ya abiria ambao walikuwa nje kubiria litengenezwe. Mariamu naye akamwita. Akaanza kuchagua. Wakati akifanya hivyo, Kamal akamshika begani.

Alipogeuka kumuangalia akamwambia. "Chukua huyo mkubwa kuliko wote hapo, nimeamua kukuchagulia."

"Mmmh! Mkubwa huyu bei yake nitaiweza?"

"Nimekwambia chukua, bei yake nitaiweza mimi!" Akajibu Kamal na Mariamu alimuelewa.

Baada ya kumchukua samaki yule mkubwa, Kamal naye akachagua yule ambaye alitaka kumnunua Mariamu.

Kwenye mkoba wake Mariamu alikuwa na sahani ya karatasi, akazitoa mbili na kumpa moja Kamal naye awekee samaki wake.

Muuza mihogo ya kuchemsha naye akapita wakanunua minne, kila mmoja akachukua miwili. Pesa zote alilipa Kamal.

"Haya sasa tule, mimi nakula samaki niliokuchangulia na mimi nakula huyu uliomchagua wewe." Kamal aliposema maneno hayo, Mariamu akamtazama kwa macho ya kumuiba mara moja na kuyaondoa, akatabasamu.

Akatoa khanga yake akatandika kwenye nyasi, wakakaa na kuanza kula. Lilikuwa ni kosa kubwa kwa Mariamu kumpa nafasi ya kuongea na kujitetea. Kesi ikawa imeishia hapo.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# COASTAL YAITAKA 'TOP 4' LIGI BARA KWA VITENDO

**Na Adam Fungamwango**

BAO la penalti lililowekwa wavuni na Lucas Kikoti dakika ya 25, liliipa ushindi wa 1-0 Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu SC iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga liliongezea mbio ya kumaliza katika nafasi ya nne msimu huu.

Ushindi huo umeifanya Coastal Union ambayo ilikuwa katika hali mbaya katika mzunguko wa kwanza kufikisha pointi 30 na kukwea hadi nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiishusha nafasi moja Tanzania Prisons yenye pointi 28.

Coastal Union imeonekana kubadilika zaidi baada ya kufanya usajili bora kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo, lakini pia kumtwaa Kocha, David Ouma, raia wa Kenya, ambaye ameonekana kuibadilisha kwa kiasi kikubwa na kuwa moja kati ya timu tishio ikicheza mechi yoyote ya ligi iwe nyumbani au ugenini.

„Tunaendelea kuwasaidia vijana, wanacheza vizuri ingawa kuna wakati wanajisahau, lakini inabidi mara kwa mara kuwakumbusha warudi katika mstari. Ihefu tumewafunga kwa sababu tumepata bahati ya kuwaona wakicheza na Yanga na wakafungwa mabao 5-0, nimeangalia wapi kwenye udhaifu wao ili tuweze kupenya na imetusaidia," alisema kocha huyo.

Baadhi ya timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na kusaka ubingwa, lakini zinapigania pia kuhakikisha zinamaliza msimu ndani ya timu nne za juu ili kujihakikishia nafasi ya kucheza mashindano ya kimataifa.

Kwa sasa Simba, Yanga na Azam zinaonekana kuhodhi nafasi tatu za juu, huku ya nne bado ikionekana iko wazi na tayari ina faida kutokana na mfumo wa Ligi Kuu Bara ulivyo.

Kanuni inasema timu mbili za juu zitakwenda kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, ya tatu michuano ya Kombe la Shirikisho, huku mwingine akipatikana kupitia Kombe la FA.

Hata hivyo, kama timu Bingwa wa Kombe la FA itakuwa moja kati ya timu mbili za juu kwenye Ligi Kuu, basi moja kwa moja, timu itakayoshika nafasi ya nne itapata nafasi ya kucheza michuano Kombe la Shirikisho Afrika.



Wachezaji wa Simba Queens wakiwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Jangwani, Dar es Salaam walipoenda kuwatembelea katika kilele cha Siku ya Wanawake Duniani kilichofanyika Machi 8, mwaka huu. **PICHA: SIMBA SC**

# Netiboli yaahidi makubwa Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Netiboli Tanzania (CHANETA), kimetamba timu yao itafanya vyema katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Dunia la mchezo huo itakayofanyika baadaye mwaka huu.

Timu hiyo ya netiboli ya umri chini ya miaka 21 iliondoka nchini jana na kuelekea Afrika Kusini ili kupeperusha bendera ya Tanzania.

Mwenyekiti wa CHANETA, Devota Marwa, alisema wameiandaa vizuri timu hiyo ili kutimiza malengo yao katika mashindano hayo ambayo yalisimama kwa muda mrefu.

„Tunaomba Watanzania waendelee kutuombea, matarajio yetu ni kurudi na ushindi nyumbani, hatuhofii timu yoyote kwa sababu wote ni wageni, „ alisema Marwa.

Aliongeza wachezaji wote wamejipanga kwenda kushindana na si kushiriki hivyo wanawaahidi Watanzania watawapa furaha.

Naye Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Charles Magunzu, ameitaka timu hiyo kwenda kupambani na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Tunaomba mkapambane mhakikishe mnarudi na ushindi, mnafahamu Tanzania ni nchi inayofanya vizuri katika nyaja za michezo kimataifa, tunaamini mtafanya vizuri," alisema Magunzu.

## Taulo lawaponza Kibu na Mzamiru

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba, Kibu Denis na Mzamiru Yassin, wametozwa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja kwa kosa la kuondoa taulo la golikipa wa Coastal Union, Ley Matampi, langoni katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyofanyika Machi 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga Mnyama akishinda mabao 2-1.

Taarifa iliyotolewa juzi imesema adhabu hiyo pamoja na nyingine, imetolewa na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) katika kikao chake kilichofanyika Machi 12, mwaka huu kwa ajili ya kupitia mwenendo na matukio mbalimbali.

"Wachezaji Kibu (Denis), na Mzamiru (Yassin) wa klabu ya Simba wametozwa fainali ya Sh. milioni moja, kila mmoja kwa kosa la kuonekana wakiondoa taulo la mlinda mlango wa Coastal Union (Matampi), lililokuwa limewekwa pembeni ya lango wakati wa mchezo husika ukiendelea, jambo linaloashiria imani za kishirikina.

Adhabu hii ni kwa kuzingatia kanuni ya 41:5 ya Ligi Kuu kuhusu udhibiti kwa wachezaji.

Wakati huo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin ,Popat', naye amepewa onyo kali kwa kosa la kuingia kwenye chumba cha kuvalia nguo na kuzungumza na wachezaji kabla ya hawajaingia uwanjani, kitu ambacho ni kosa kwa kuzingatia kanuni ya 17:50 na 17:60 ya Ligi Kuu kuhusu utaratibu wa mchezo.

Popat alifanya kosa hilo wakati Azam FC inacheza dhidi ya Dodoma Jiji, mechi iliyofanyika Machi 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Azam FC pia imepigwa faini la ya Sh. milioni moja kwa kosa la wachezaji wake kuchelewa kurudi uwanjani baada ya mapumziko katika mechi dhidi ya Tabora United iliyochezwa Februari 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora huku kocha wao, Yossouph Dabo, akitozwa faini kama hiyo kwa kosa la kutoa lugha chafu na maneno ya kashfa kwa waamuzi baada ya kumalizika kwa mchezo huo.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko katika hatua ya lala salama inatarajia kuendelea tena kesho kwa Azam FC kukutana na vinara na mabingwa watetezi, Yanga.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CHELSEA YAMHOFIA OSIMHEN**

CHELSEA inahofia watamkosa mchezaji wa Napoli, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, katika uhamisho wa majira ya joto, huku Paris St-Germain na Arsenal zikiongeza juhudi katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji huyo mahiri wa timu ya taifa ya Nigeria. ***(Teamtalk)***

**RASHFORD BADO YUPO**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 26, hatarajiwi kuhamia PSG msimu huu wa joto kufuatia ripoti atachukua nafasi ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe (25). ***(Sky Sports)***

**UNITED KUMUUZA GREENWOOD**

KLABU ya Getafe haitampata, Mason Greenwood zaidi ya muda wake wa mkopo kwa sababu Manchester United wameamua kumuuza mshambulijai huyo wa England mwenye umri wa miaka 22. (***Marca)***

**DE BRUYNE NJIA MOJA**

KLABU ya Manchester City imeamua kuahirisha mazungumzo ya kumpa mkataba mpya kiungo wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, mwenye umri wa miaka 32, ambaye amebakiza zaidi ya mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa. ***(Football Insider)***

**VILLA KUMBAKIZA LUIZ**

KLABU ya Aston Villa ina imani itaweza kumbakisha kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Douglas Luiz, licha ya Arsenal kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(90 Min)***

**SOUTHGATE, ENGLAND KUTETA**

KOCHA wa England, Gareth Southgate, amefichua amekiambia Chama cha Soka England (FA), atafanya mazungumzo kuhusu mustakabali wake hadi baada ya Euro 2024. ***(Mirror)***

**MANCHINI KUTUA NEWCASTLE**

KOCHA wa zamani wa Manchester City na sasa Saudi Arabia, Roberto Mancini, analengwa na Newcastle United iwapo wataamua kuachana na Eddie Howe msimu huu wa joto. ***(HITC)***

**ASHWORTH ATAKIWA HARAKA**

KLABU ya Newcastle inataka kuharakisha kuondoka kwa Dan Ashworth kwenda Manchester United huku Mkurugenzi wa Michezo wa Monaco, Paul Mitchell, akiongoza orodha fupi ya wagombea kuchukua nafasi yake. ***(Telegraph)***

**YORO ATAKIWA CHELSEA**

CHELSEA imeonyesha nia ya kumnunua beki wa kati wa Lille, Mfaransa Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, wakati wa majira ya joto, huku wakipima nafasi ya beki wa Brazil, Thiago Silva (39). ***(Standard)***

**CUBARSI AGOMBEWA EPL**

MANCHESTER United, Chelsea na Arsenal zinavutiwa na kijana wa Barcelona na Hispania, Pau Cubarsi, mwenye umri wa miaka 17. ***(Football Espana)***

**DIOMANDE ATAJWA SOKONI**

NEWCASTLE United na Arsenal zimeimarika katika harakati zao za kumtafuta beki wa kati wa Sporting Lisbon, Ousmane Diomande, mwenye umri wa miaka 20, huku Chelsea wakihitaji kuuza wachezaji kabla ya kuthibitisha kuwasili kwa wachezaji wapya msimu huu. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VINICIUS JR, MADRID MAMBO YAMEHARIBIKA

●●●Mshambuliaji huyo aingia katika mgogoro na klabu akidai...

**MADRID, Hispania**

CHAPISHO la kwenye mtandao wa kijamii la Real Madrid lilisababisha mtafaruku mkubwa kati ya klabu hiyo na nyota wake, Vinícius Júnior kabla ya mechi dhidi ya Valencia iliyochezwa Machi 2, mwaka huu, vyanzo vimemdokeza mwandishi, Gustavo Hofman wa ESPN.

Chapisho la Instagram lilikuwa na picha ya Vinícius akibusu beji ya Real Madrid.

Hata hivyo, chini yake, picha ilijumuisha kibandiko kilicho na nembo ya ma DJ wawili maarufu wa Israeli 'Vini Vici,' ambacho kinatumia mchoro unaoonyesha mabadiliko ya binadamu kutoka nyani hadi DJ.

Wakati chapisho hilo lilibaki mtandaoni kwa dakika 30, lilionekana kumkera sana Vinícius kwa sababu ilikuwa kama likimdhalilisha kwa kumfananisha na nyani.

Fowadi huyo wa Brazil alikabiliana na uongozi wa klabu hiyo kwa hasira, akitaka maelezo na hata kutishia kutoshiriki mechi dhidi ya Valencia, kwa mujibu wa vyanzo hivyo.

Habari kuhusu mpasuko kati ya Madrid na Vinícius iliripotiwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Relevo hapo jana.

Baada ya Vinícius kuja juu, Mkurugenzi Mtendaji wa Real Madrid, José Ángel Sánchez, aliingilia kati, vyanzo hivyo viliongeza.

Alilenga kumtuliza na kufafanua hali ilivyo baada ya mshambuliaji huyo kueleza kutoridhika akizingatia kampeni yake inayoendelea dhidi ya unyanyasaji wa kibaguzi wa rangi katika soka.

Sánchez alifaulu kumtuliza Vinícius na kuahidi kulifanyia uchunguzi wa kina, huku akizingatia sera ya Madrid inapinga kwa nguvu zote ubaguzi wa rangi kwenye mpira wa miguu.

Licha ya tukio la kabla ya mechi, Vinícius alianza mchezo dhidi ya Valencia kwenye Uwanja wa Mestalla, akifunga mara mbili na kupata sare ya 2-2.

Hata hivyo, Real Madrid ilikataa kuzungumzia tukio hilo ilipoulizwa na ESPN.

# BEN WHITE AKATAA KUICHEZEA ENGLAND

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amefichua Ben White wa Arsenal amekataa kuichezea timu hiyo.

Juzi Southgate alitaja kikosi cha wachezaji 25 kwa ajili ya mechi zijazo za kirafiki dhidi ya Brazil na Ubelgiji huku Jarrad Branthwaite wa Everton na winga wa Newcastle, Anthony Gordon, wote wakichaguliwa kwa mara ya kwanza pamoja na Ivan Toney akiitwa baada ya kufungiwa kwake kwa miezi nane kwa kukiuka sheria za kamari.

Lakini licha ya kuumia kwa mabeki kadhaa wakiwamo Kieran Trippier, Trent Alexander-Arnold, Reece James na Marc Guehi, White hakujumuishwa katika kikosi cha England.

Mlinzi huyo amekuwa bora katika kikosi cha Arsenal ambacho kinaongoza Ligi Kuu England na kimetinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

White alichaguliwa kwenye Kombe la Dunia la 2022, lakini aliondoka kambini mapema akitaja "sababu za kibinafsi" huku kukiwa na ripoti za ugomvi kwenye mazoezi kati yake na msaidizi wa Southgate, Steve Holland.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 hajajumuishwa katika kikosi tangu michuano ya Kombe la Dunia nchini Qatar na alipoulizwa iwapo sasa atamuita, Southgate alisema: "Angalia, ni swali kabisa unapaswa kuuliza kwa sababu ni wazi kabisa yupo kwenye kiwango kizuri. Siwezi kukaa hapa na kusema hastahili ndani ya kikosi changu.

"Sisi, (Mkurugenzi wa Ufundi wa FA) John McDermott, tulipigiwa simu na (mkurugenzi wa ufundi wa Arsenal) Edu wiki iliyopita na kusema Ben hataki kujumuishwa kwenye kikosi cha England kwa wakati huu.



"Kwangu mimi, hiyo ni aibu kubwa. Ni mchezaji ninayempenda sana. Ni mchezaji tuliyemchukua kwenye michuano ya Euro alipokuwa Brighton, mchezaji tuliyempeleka kwenye Kombe la Dunia.

"Nilizungumza naye baada ya Kombe la Dunia kule Qatar kwa sababu nilitaka kumchagua na ni wazi kulikuwa na uzembe upande wake. Sijui kwa nini ni hivyo lakini lazima niheshimu maamuzi yake.

"Nataka kuacha milango wazi kwake kwa sababu ni mchezaji mzuri. Nadhani ni mchezaji anayeweza kuleta mabadiliko kwa England.

"Lakini kutoitwa kwake hakuna kitu kingine kati yetu, na pia kamwe hakuna suala na Steve Holland.

"Watu wanaweza kuongea na kunihusishwa mimi, lakini lazima nisemehayo ni ambayo ni ya uongo.

"Angekuwa kwenye kikosi hiki. Lakini mwenyewe hataki, hivyo lazima nitangaze wazi."

## Salah aweka rekodi mpya

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah aliweka rekodi ya kihistoria ya mabao kwa Liverpool alipofunga bao la tatu wakati timu hiyo ikiiangamiza Sparta Prague kwa kichapo cha mabao 6-1 kwenye mchezo wa Ligi ya Europa wa hatua ya 16 bora pale kwenye dimba la Anfield na kutinga robo fainali juzi usiku.

Bao lenyewe halikuwa la maana sana usiku huo, huku vijana wa Jurgen Klopp wakiwa tayari walikuwa mbele kwa 2-0 wakati huo dakika 10 tu za mchezo wa mkondo wa pili wa hatua ya 16 bora, wakiwa tayari wameshinda magoli 5-1 katika mji mkuu wa Czech wiki iliyopita.

Lakini ilichowakilisha kilikuwa zaidi kuhusu maisha ya Salah kwa Liverpool kwa ujumla na ubora wa ajabu ambao ameonyesha tangu alipoanza kucheza Anfield mnamo 2017.

Ni msimu wa saba mfululizo kwa supastaa huyo wa Misri kufikisha mabao 20 katika michuano yote, jambo ambalo hakuna mchezaji mwingine yeyote katika historia ya Liverpool aliyewahi kuifikia.

Rekodi ya awali ya misimu sita mfululizo ya mabao 20 ambayo Salah aliisawazisha mwaka jana, iliwekwa na gwiji wa miaka ya 1980, Ian Rush.

Rush aliweka reodi ya kufunga mabao 27 hadi 40 kwa msimu kati ya 1981 na 1987. Mbio zake hatimaye zilivunjwa na uhamisho wa kwenda Juventus ambao ulimfanya ashingwe kuzoea maisha ndani na nje ya uwanja kwenye Serie A.

Mshambuliaji huyo wa Wales alirejea tena Liverpool na kufurahia misimu mitatu zaidi ya kufunga mabao 20 kila msimu katika kipindi cha miaka nane na aliondoka Anfield kwa uzuri mwaka 1996 akiwa na umri wa miaka 34.

Maoni yaliibuka wakati Liverpool ilipotumia zaidi ya pauni milioni 30 kumnunua Salah mnamo 2017, na kurejea katika soka ya Uingereza baada ya muda mfupi usio na mafanikio akiwa Chelsea.

Alikuwa amerejesha sifa yake nchini Italia akiwa na Roma, lakini akapiga hatua mpya kwa msimu wa mabao 44 akiwa na jezi nyekundu ya vijogoo hao wa Anfiled.

Salah yupo nafasi ya tano kwa kama mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo akiwa na mabao 206, mbele ya magwiji Sir Kenny Dalglish na Robbie Fowler, na pia mchezaji pekee asiye Mwingereza katika 10.

***

## De Bruyne atemwa Ubelgiji

**BRUSSELS, Ubelgiji**

KEVIN De Bruyne ameachwa nje ya kikosi cha Ubelgiji kwa ajili ya mechi za kimataifa baada ya kupata majeraha ya nyonga.

Akiwa amekosa miezi minne ya kampeni kutokana na jeraha la msuli wa paja, De Bruyne amekuwa katika hali nzuri tangu arejee Januari na sasa ana asisti 13 katika mechi 14 za mashindano yote pale Manchester City.



Asisti yake ya hivi karibuni ilikuja katika sare ya 1-1 dhidi ya Liverpool.

Na sasa Kocha wa Ubelgiji, Domenico Tedesco, amefichua De Bruyne hayuko sawa kabisa na ameachwa nje ya kikosi cha kimataifa kutokana na hilo.

"Amekuwa akicheza na tatizo la paja katika mechi chache zilizopita," alisema Tedesco.

"Nilizungumza na daktari na Kevin na tukaamua ni hatari kubwa kumjumuisha kwenye kikosi.

"Ni bora kumpa muda wa kupona vizuri akiwa Manchester City halafu awe tayari kwa Euro."

De Bruyne hataonekana katika mechi ya robo fainali ya Kombe la FA wikendi hii dhidi ya Newcastle United kutokana na tatizo hilo.

Baada ya mapumziko ya kimataifa, City watarejea uwanjani wakiwa na mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya wapinzani wao Arsenal kwenye Uwanja wa Etihad.

Guardiola atamtaka De Bruyne awe fiti kwa ajili ya mchezo huo na hivyo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 ambaye ataachwa nyumbani wakati wa mapumziko ya kimataifa atakuwa msaada mkubwa kwa bosi wa City.

## HABARI MICHEZO

# AZAM FC YATAJWA KUTUMA MAOMBI KUMSAJILI MAYELE

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umepeleka maombi kwa klabu ya Pyramids ya Misri ili kuinasa saini ya mshambuliaji wake ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Fiston Mayele, imefahamika.

Hatua ya kutaka huduma ya Mayele imetokana na mshambuliaji wa timu hiyo, Prince Dube, kutangaza anahitaji kuvunja mkataba na matajiri hao wa Chamazi ili kwenda kutafuta changamoto mpya.

Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe zinasema Azam FC imekubali kumlipa mshahara wa Dola za Marekani 15,000 kwa mwezi ili kupata huduma ya Mayele huku ikitajwa huenda Dube akajiunga na Simba au Al Hilal ya Sudan.

Chanzo chetu kutoka Azam kiliendelea kusema uamuzi wa kumfuata Mayele umetokana na Mkongomani huyo kuonyesha nia kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara na tayari ameshaiandikia barua Pyramids akiweka wazi uamuzi huo.

Kiliongeza sababu kubwa ya Mayele kutaka kuondoka Misri ni changamoto ya kutopata nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha kwanza kama alivyotarajia.

"Tumepeleka ofa juu ya kumhitaji Mayele kwa ajili ya kuja kuziba nafasi ya Dube, ameamua kuondoka kwenye timu na kudai kuachwa, tumetangaza ofa na tayari Simba na Al Hilal wameonyesha nia ya kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo.

Tunahitaji kuimarisha kikosi chetu kwa ajili msimu ujao, tunataka kuwa na timu imara, tunaimani Mayele ni sahihi kwetu, kuipata huduma yake ni jambo jema kwa sababu mshambuliaji wetu (Dube), amejiondoa mwenyewe katika timu," kilisema chanzo chetu.

Naye Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin ‚Popat', amekiri kupokea ofa kutoka Simba na Al Hilal na kuongeza bado milango iko wazi.

"Uongozi unazifanyia tathmini ofa hizo za klabu mbili ili kuona ipi inafaa kwao, lakini pia tunafungulia milango kwa klabu nyingine zinazohitaji huduma ya Dube, kuhusu usajili tutaimarisha kikosi kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi," Popat alisema.

Mayele aliyetua Pyramids akitokea Yanga alikuwa na msimu mzuri na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa ni mmoja waliosaidia kucheza fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Wachezaji wa Coastal Union wakishangilia baada ya kupata bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu SC iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga juzi. Coastal ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Hat-trick 5 zapigwa Bara

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya ‚hat-trick' tano zimefungwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia raundi ya 20, ikibaki moja kutimiza idadi ya zilizofungwa kwenye msimu uliopita.

Kwa mujibu wa dawati letu la rekodi na takwimu, Tabora United imeruhusu kupigwa ‚hat-trick' mbili, zote wakifungwa kwenye Uwanja Azam Complex, Dar es Salaam, uwanja ambao umezaa ‚hat-trick' tatu.

Mapema wiki hii kwenye Uwanja wa Azam Complex, straika wa KMC, Waziri Junior, alifunga hat-trick na kuongoza timu yake kutoa kichapo cha mabao 4-2 dhidi ya Tabora United, akitimiza ya tano.

Msimu huu, mmoja wa vinara wa mabao kwenye Ligi Kuu, Feisal Salum ‚Fei Toto', akiwa na mabao 12 mpaka sasa, ndiye mchezaji wa kwanza kutupia, alipofanya hivyo katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Tabora United.

Wachezaji wengine ni Baleke aliyekuwa akichezea Simba, Stephane Aziz Ki wa Yanga na Kipre Junior wa Azam FC.

Kipre alifunga, Novemba 24, mwaka jana, dakika ya 29, 43 na 62, akiiongoza Azam kushinda mabao 5-0 dhidi ya Mtibwa Sugar, mechi ikichezwa Uwanja wa Azam Complex.

Beleke alifunga ‚hat-trick' yake dakika ya sita, 10 na 40, Septemba 21 mwaka jana, Simba ikiifunga Coastal Union mabao 3-0, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, huku Aziz Ki, akifanya kama hivyo, Oktoba 13, mabao ya dakika ya nane, 68 na 71, akiiwezesha Yanga kushinda mabao 3-2 dhidi ya Azam, mechi ikichezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Yanga SC yawapoteza Mamelodi Chamazi

INATOKA UK. 24

Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema safari hii ‚mpango kazi' walionao ni kutumia vizuri uwanja wa nyumbani kumaliza mechi.

Ahmed alisema kosa walilolifanya miaka ya nyuma ni kutotumia vyema mechi za nyumbani, hivyo wakawa na kazi ngumu ugenini.

„Safari hii mpango wetu ni kutumia kwa asilimia 100 uwanja wa nyumbani, yaani kumaliza mechi hapa Dar es Salaam. Katika robo fainali nne za CAF tulizocheza hatukutumia ipasavyo mechi za nyumbani, ingawa siyo rahisi, lakini inawezekana," alisema Ahmed.

Aliongeza Simba inataka kuweka rekodi ya kuitoa Al Ahly katika hatua ya robo fainali ambayo mara nyingi huishia fainali au kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

„Huwezi kumkuta Al Ahly ameishia hatua ya robo fainali, akipita katika makundi basi anakwenda hadi fainali, hapo ndio mwisho wake, atachukua kombe au atafungwa, lakini safari hii tunataka kuweka rekodi ya kumtoa kwenye hatua hii," meneja huyo alisema.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wameshaanza maandalizi ya mechi yao hiyo ya kimataifa huku wakichukua tahadhari zote za kukwepa udukuzi kutoka kwa Mamelodi Sundowns.

„Hata mechi hii dhidi ya Geita Gold hatukucheza katika kile kiwango chetu kwa sababu tunajua kuna watu wametumwa kutuchunguza, wamenoa," alisema Kamwe.

## Kilichomwondoa Job Taifa Stars

INATOKA UK. 24

Kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Morocco, alisema ameita kikosi hicho kulingana na matakwa ya mfumo wake kuelekea michezo hiyo miwili.

Morocco alisema Job alifanya makosa kwa sasa hawezi kuzungumzia hilo huku akiongeza kila mchezaji anatakiwa kuheshimu uamuzi wa benchi la ufundi na hasa pale unapopewa majukumu.

"Sitaki kumzungumzia Job, hao wanaomwongelea hawamsaidii, nikisema nizungumze kuhusu nyota huyo basi tutampoteza katika ramani ya mpira, mchezaji mzuri na bado yupo katika kikosi cha Stars," alisema Morocco.

Katika mechi hizo mbili za kirafiki, Stars itamkosa pia nahodha wake, Mbwana Samatta, ambaye aliomba kutojumuishwa kwa sasa.

Michezo

Jumamosi Machi 16, 2024

Nipashe

Vinicius Jr, Madrid mambo yameharibika UKURASA 21



# Kilichomwondoa Job Taifa Stars chaanikwa

**Na Saada Akida**

UTOVU wa nidhamu unatajwa ndio sababu pekee iliyomwondoa katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), beki wa Yanga, Dickson Job, imefahamika.

Kikosi cha Stars kinatarajia kuingia kambini kesho kwa ajili ya kujiandaa na michezo miwili ya kimataifa inayotambuliwa na Kalenda ya FIFA dhidi ya Bulgaria na Mongolia na.

Mechi hizo zitachezwa kati ya Machi 22 na 25, mwaka huu nchini Azerbaijan.

Taarifa kutoka katika kikosi cha Taifa Stars zinasema Job alionyesha utovu wa nidhamu baada ya kukataa kucheza mechi ya mwisho ya michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Chanzo hicho kilisema kitendo cha kugomea kucheza mechi hiyo hakikuwa cha kizalendo na ndio sababu kuu ya kutemwa katika kikosi hicho.



"Hakuna sababu nyingine zaidi ya utovu wa nidhamu, alikosa uzalendo ukizingatia katika mchezo na Congo kwenye fainali za AFCON zilizofanyika Ivory Coast ulikuwa ni muhimu zaidi, Job alitakiwa kucheza beki namba mbili, alikataa kucheza nafasi hiyo badala yake akacheza Lusajo (Mwaikenda).

Lakini baadaye Job aliendа kuomba msamaha kwa kocha hali iliyopelekea kupewa adhabu hiyo ya kuondolewa kwenye kikosi na hatakuwa sehemu ya nyota watakaosafiri Jumatatu kuelekea Azerbaijan," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza suala la beki huyo lilipelekwa rasmi kwa viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na uamuzi mwingine utafanyika kutoka kwa mabosi hao wa soka nchini.

INAENDELEA UK. 23

# YANGA YAWAPOTEZA MAMELODI CHAMAZI

## ●●●Yawashtukia mashushushu wake, Simba yaandaa 'mpango kazi' CAF...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akiwashtukia wapinzani wao kwa kubadilisha kikosi, Simba itaanza kucheza mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri Machi 29, mwaka huu huku Yanga ikishuka dimbani siku inayofuata kuwavaa Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini.

Mechi zote mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika zitachezwa kuanzia saa 3:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Gamondi alisema alilazimika kubadilisha mfumo katika kikosi chake wakati anacheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold kwa sababu alifahamu Mamelodi Sundowns imetuma ‚mashushu' kwa ajili ya kuwapeleleza.

Gamondi alisema anatambua kufuatiliwa na wapinzani wao na sababu hiyo ndio ilipeleka kufanya mabadiliko machache ya kikosi kwa kuwaanzisha baadhi ya wachezaji ambao mara kadhaa hutokea benchi katika mechi hiyo iliyomalizika wakipata ushindi wa bao 1-0.

Kocha huyo alisema anaimani uwanjani hapo kulikuwa na watu kutoka Afrika Kusini waliofika kwa kazi moja ya kuwachunguza na anajua watakuwepo pia katika mchezo unaofuata watakapokutana na Azam FC hapo kesho.

Alisema anafurahi kuona wanaendelea kuvuna pointi tatu muhimu na sio anajua kila siku huwezi kumfunga mpinzani mabao kuanzia manne au matano.

"Lazima umheshimu mpinzani, unakutana na timu ambayo imejipanga kama ilivyo kwa Geita Gold FC walicheza vizuri, kwa sasa tunahitaji kupumzika, nawapongeza wachezaji wamejituma na walipambana.

Lazima tukiri mpinzani wetu alikuwa mgumu na tumemaliza mechi hiyo sasa ni kuwapa muda wachezaji wa kupumzika na baadaye kuanza kufikiria maandalizi ya mchezo dhidi ya Azam FC," alisema Kocha huyo.

Aliongeza wachezaji wake hawajapata muda wa kutosha wa kupumzika tangu waliporejea nchini wakitokea Misri katika mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), inaonyesha mechi za marudiano za ugenini zote zitachezwa Aprili 5, mwaka huu.

Akizungumzia hilo, Meneja

INAENDELEA UK. 23



## ROBO FAINALI UEFA

| | | |
|---|---|---|
| Arsenal | vs | Bayern Munich |
| Atletico.M | vs | B. Dortmund |
| Real Madrid | vs | Man City |
| PSG | vs | Barcelona |

UEFA CHAMPIONS LEAGUE

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >